**Ripoti ya kila siku**

# MTETEZI YA KILA SIKU ZA WAKRISTO

Mukutano Mkuu ya Kanisa ya Muungano ya Kimethodisti

Charlotte, North Carolina | Friday, April 26 2024 | Vol. 5, No. 4

## Contents

Ijjuma, 26 Aprili . . . . . 2015
Memoranda ya Baraza la Mahakama (Memeradum du Conseil Judiciare) No. 1495 . . . . . 2016
Uamuzi wa Baraza la Mahakama 1496 . . . . . 2016
Errata (Makosa) 26 Aprili . . . . . 2018
Repoti ya Ufuatuliaji Usawa wa GCORR DCA 4 . . . . . 2019
Ripoti ya Ufuatiliaji ya GCSROW Aprili 26, 2024 . . . . . 2021
Plan of Organization and Rules of Order . . . . . 2023
Calendar . . . . . 2065

## Ijjuma, 26 Aprili

07:00 - Kamati juu ya Ajenda na Kalenda

- Kamati ya Kumbukumbu

07:30-18:30 - Kujiandikisha (Watu wote)
08:00-08:45 - Ibada
08:45-10:20 - Kikao cha makutano

- Maombi ya Kufunguwa mukutano
- Ripoti ya ukaguzi (dakika 3)
- Ripoti ya Meza Unganisho (dakika 20)
- Ripoti ya Kamati za Utawala
- Mambo toka kwa Kalenda

10:20-10:40 – Mapumuziko
10:40-12:30 – Kamati ya Sheria
12:30-13:30 – Chakula cha mchana
13:30-16:00 – Kamati ya Sheria
16:00 16:20 – Mapumuziko
16:20-18:20 – Kamati za Sheria
17:00 – Kikomo ya kila siku Uchapishaji wa DCA
18:20-18:30 – Maombi ya jioni (Kamati za Sheria)
18:30 – kuhirisha

# Memoranda ya Baraza la Mahakama (Memeradum du Conseil Judiciare) No. 1495

## Aprili 22, 2024

Kutona na: Ombi la Uamuzi wa Tamko kutoka kwa Baraza la Maaskofu kuhusu Maana, Matumizi, na Athari ya ¶¶ 55 na 2602.1 ya Kitabu cha Nidhamu cha 2016.

## Taarifa ya Ukweli

Mnamo Aprili 10, 2024, Baraza la Maaskofu liliwasilisha kwa Baraza la Mahakama Ombi la Uamuzi wa Maamuzi yenye maswali yafuatayo:

1. Je, mustali huu "Muda wa afisi wa mwanachama utakuwa miaka minane" katika ¶ 2602.1 ina maana kwamba mtu aliyechaguliwa kwa Baraza la Mahakama katika Mukutano Mkuu wa 2016 ametumikia muhula mmoja wa miaka minane na lazima agombee kuchaguliwa tena katika Mkutano Mkuu wa 2020? utakaofanyika mwaka wa 2024 ikiwa mtu huyo anataka kuendelea kuhudumu katika Baraza la Mahakama?
2. Je, ¶ 55 ya Nidhamu inaipatia Baraza Kuu mamlaka ya kutunga sheria ya kurekebisha ¶ 2602.1 na kuamua kama mtu aliyechaguliwa kwa Baraza la Mahakama katika Mukutano Mkuu wa 2016 amehudumu kwa muhula mmoja wa miaka minane na lazima agombee tena uchaguzi katika 2020 Mkutano Mkuu utakaofanyika 2024?

## Ufafanuzi

Baraza la Mahakama wanakataa mamlaka katika eno hilo. Katiba inatoa katika ¶ 55: "Kutakuwa na Baraza la Mahakama. **Mkutano Mkuu** utaamua idadi na sifa (qualifications) za wanachama wake, mihula yao ya ofisi, na njia ya uchaguzi na ujazaji wa nafasi zilizoachwa wazi." [Mkazo imeonzwa]

Aprili 22, 2024

# Uamuzi wa Baraza la Mahakama 1496

## Aprili 22, 2024

KUTOKANA NA: Ombi la Uamuzi wa Matangazo Kuhusu Aya ya 710.4 ya Kitabu cha Nidhamu cha 2016.

## Ufafanuzi

Iwapo watateuliwa na kuchaguliwa katika Mkutano MKuu wa 2020 lililoahirishwa mwaka wa 2024, wanachama wa mashirika makuu ambao walichaguliwa kwa mara ya kwanza kwa mda wa miaka minne katika Mkutano MKuu wa 2016

wanaweza kuchaguliwa kuhudumu mda wa pili wa miaka minne.

## Taarifa ya Ukweli

Swali lililo ulizwa kwa Baraza la Mahakama na Baraza la Maaskofu katika Ombi lake la Uamuzi wa neno linauliza: Je, ¶ 710.4 inaruhusu mjumbe wa kupiga kura wa wakala mkuu aliyechaguliwa katika Mkutano Mkuu wa 2016 kuchaguliwa kutumikia mda  ya pili kuanzia mwisho? ya Mkutano Mkuu wa 2020 utakaofanyika 2024?

## Mamlaka

Baraza la Mahakama lina mamlaka katika kesi hii kulingana na ¶ 2010.2b.

## Uchambuzi na Sababu

Sheria ya Kanisa inatoa jibu kwa swali lililowekwa kwenye Baraza la Mahakama. Washiriki wa upigaji kura wanaohusika hawawezi kuhudumu kwa zaidi ya mda miwili mfululizo ya miaka minne, ya kwanza ambayo ilianza katika mkutano wa kwanza wa wakala wao kufuatia Mkutano Mkuu wa 2016 wa Portland. Wanachama hawa bado wanatumikia mda wao wa kwanza wa miaka minne (ingawa imedumu kwa miaka minane) kwa sababu tangu mkutano huo wa kwanza haujafanyika Mkutano Mkuu uliofuata na hakuna aliyeteuliwa, kuchaguliwa na kusimikwa kuchukua nafasi zao. Iwapo watateuliwa na kuchaguliwa kwa mda mwingine katika mkutano Mkuu lililoahirishwa kwa 2020 linalofanyika mwaka wa 2024, wataanza mda wao wa pili wa miaka minne uliotolewa katika Â¶ 710.4 ku mkutano wa kwanza wa wakala mkuu kufuatia Mkutano Mkuu ya 2020 lililoahirishwa huko Charlotte.

## Uamzi

Iwapo watateuliwa na kuchaguliwa katika Mkutano Mkuu ya 2020 lililoahirishwa mwaka wa 2024, wanachama wa mashirika makuu ambao walichaguliwa kwa mara ya kwanza kwa Robo wa miaka minne katika Mkutano Mkuu ya 2016 wanaweza kuchaguliwa kuhudumu mda wa pili wa miaka minne.

Aprili 22, 2024

## Maoni Yanayopingana

Ombi hili la Uamuzi wa Tamko kimsingi linaomba kama, chini ya ¶ 710.4, mwanachama wa kupiga kura wa wakala mkuu ambaye alichaguliwa wakati wa Mkutano Mkuu wa 2016 anastahili kuchaguliwa tena katika Mkutano Mkuu huu.

Swali hili halionyeshi masuala yoyote ya kikatiba bali ni uamuzi wa kisheria ambao unapaswa kufanywa na Mkutano Mkuu. Angalia, e.g kushikilia kwenye JCD 1310. Tazama pia JCD 1303.

Nidhamu inatoa katika ¶ 2608.2 kwamba:

Baraza linaweza kukataa kupokea rufaa au ombi la uamuzi wa tamko katika hali yoyote ambayo litaamua kwamba halina mamlaka ya kuamua suala hilo.

Baraza la Mahakama lilipaswa kuwa limekataa mamlaka kama lilivyofanya katika Mkataba 1495 kuhusu muda wa ofisi kwa wajumbe wa Baraza la Mahakama. Haya ni mambo yatakayoamuliwa na baraza la kutunga sheria la dhehebu, Mkutano Mkuu, ambalo litakusanywa kwa chini ya saa 24. Katiba inaeleza yafuatayo:

**¶ 16. Kifungu cha IV**. **Mkutano Mkuu utakuwa na mamlaka kamili** ya kutunga sheria juu ya mambo yote yenye uhusiano tofauti, na katika utekelezaji wa mamlaka haya itakuwa na mamlaka kama ifuatavyo:

4. Kuandaa, Kukuza , na Usimamizi wa kazi ya Kanisa nje ya Marekani [Kamati ya Mkutano Mkuu]

8. Kuanzisha na kuelekeza mashirika yote yanayohusiana la Kanisa na kutoa bodi kwa ajili ya ukuzaji na usimamizi wao.

13. Kyanzisha tume kama hizo kwa ajili ya kazi ya

jumla ya Kanisa kama inavyoweza kuonekana kuwa inafaa.

14. **Kupata haki na mapendeleo ya uanachama Katika wakala, programu** wa Methodisti bila kujali rangi, jinsia au hadhi.

[mkazo umeongezwa]

Baraza la Mahakama lazima siku zote liwe makini na liepuke kufanya yale ambayo yangenyakua mamlaka ya Mkutano Mkuu. Vile vile, Baraza la Maaskofu linaweza kusaidia katika suala hili kwa kuepuka kishawishi cha kufanya maombi ya maamuzi ya tamko wakati hakuna masuala ya kikatiba na Mkutano Mkuu unakaribia kuitishwa. Kwa kutangaza kwamba kipindi cha miaka minane [2016-2024] kinajumuisha robo ya miaka minne, kwa maoni yangu, ni sheria. Hii inakiuka na kudhoofisha mamlaka ya kikatiba ambayo yamewekwa pekee na ya kipekee katika Mkutano Mkuu.

Kinachotia wasiwasi mkubwa ni lugha inayotumika katika Maombi haya ya Maamuzi. Kuna nyakati nyingi ambapo msemo Uliohairishwa wa **Mkutano Mkuu wa 2020 utakaofanyika 2024** unaonekana kwenye Ombi. Uamuzi wa Baraza la Mahakama 1451 ulitumia kishazi hicho katika kushughulikia suala la watu ambao wangehudumu kama wajumbe wa Mkutano Mkuu huu wa 2024. Kinyume na suala la watu ambao wamekuwa wakihudumu katika bodi kuu na mashirika tangu 2016, watu ambao walichaguliwa kuhudumu kama wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 2020 bado hawajahudumu katika uwezo huo. Kwa vyovyote vile, Maamuzi 1451 na 1472 yalibadilishwa na kufafanuliwa na Memorandum 1485 ambamo Baraza la Mahakama liliamua haswa kwamba Mkutano Mkuu huu **ni kikao cha kawaida cha 2024 cha Mkutano Mkuu** na pia ilifanya kikao kijacho cha kawaida ambacho kufuatia kikao cha kawaida cha 2024 kitakuwa Mkutano Mkuu wa 2028. Katika matukio matatu tofauti, Baraza la Mahakama lilirejelea "**kikao cha kawaida cha 2024 cha Mkutano Mkuu.**"

Mkutano Mkuu ndio chombo chenye mamlaka ya kuamua mambo haya. Ikiwa Mkutano Mkuu unataka uamuzi kutoka kwa Baraza la Mahakama basi Mkutano Mkuu wenyewe unaweza kuuliza maswali kama hayo. Ninaamini kwamba tunaweza kuhatarisha kupunguza mamlaka na usawa wa mamlaka tunapochukua hatua ambazo kimsingi zinatanguliza mamlaka ya chombo kingine ndani ya muundo wetu wa madhehebu, ikiwa ni pamoja na ushiriki kamili na sawa wa waumini (ambao haupo kabisa wakati chombo hicho kinaundwa kikamilifu. wa makasisi na/au Maaskofu). Ninaomba kwamba tutajitahidi kuwa wasikivu zaidi na wenye ufahamu katika hali kama hizi.

Beth Capen Aprili 22, 2024

# Errata (Makosa) 26 Aprili

## Makosa katika ADCA

Katika ADCA Juzuu ya 3, uk. 1598, Sababu ya Ombi 21073-IC-¶1712 haiku kweli. Mantiki iliyochapishwa ina maandishi kutoka kwa ombi tofauti, haihusu Alama za Urithi, na inapaswa kupuuzwa wakati wa kuzingatia Ombi 21073.

P. 1659, ombi 20938 limeorodheshwa kimakosa kuwa linatoka kwa Halmashauri Kuu ya Elimu ya Juu na Wizara. Ni kutoka kwa Ashley Davis, Mkutano wa Mwaka wa Alabama-West Florida.

## Makosa katika DCA

Baku la 5, Na. 3, p. 2002. Tarehe ya Ripoti ya Kamati ya Kanuni imeorodheshwa kimakosa kuwa Aprili 25. Tarehe sahihi ni Aprili 23.

p. 2006. Jina la Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya 4 katika kamati ya Mikutano limeorodheshwa kimakosa kama Jason Nelson. Jina sahihi ni Jan Nelson.

P. 2007.

Makamu Mwenyekiti wa kamati ya Kanisa la Mtaa ameorodheshwa kimakosa kama Jennifer Choi. Jina sahihi ni Jennifer Cho.

Jina la mwisho la Katibu wa kamati ya Kanisa la Mtaa halipo. Jina sahihi ni Alvin Makunike.

# Repoti ya Ufuatuliaji Usawa wa GCORR DCA 4

Wamethodisti wa Muungano kote ulimwenguni wameunganishwa pamoja katika agano la kuunganisha ambalo tunasaidiana na kuwajibisha kila mmoja kwa ufuasi mwaminifu na misheni. Kwa kushikilia kikamilifu umoja wa muunganisho na uhuru wa ndani, tunatafuta kutangaza na kujumuisha injili kwa njia zinazowajibika kwa njia zetu maalum kuhusiana na kitamaduni na kijamii huku tukidumisha “mtandao muhimu wa mahusiano shirikishi” (*Kitabu cha Nidhamu* ¶132)

Ugumu na hitaji la maono haya ya kikanisa kuhusu jinsi tunapaswa kuishi katika uhusiano ulionekana na kusisika dhahiri wakati wa kikao cha Alhamisi asubuhi. Wajajumbe kwanza walikubali masuala ya kalenda yanayohusiana na kuunga mkono kikanda kwa ulimwengu wote. Hiyo ilibadilika kuwa wakati muhimu sana wa kusikia na kisha kukubali ombi la Mkutano (Conference) wa Eurasia kuwa huru kwa amani kutoka Kanisa la United Methodist. Mara baada ya hapo, wajumbe walifanya majadiliano juu ya mabadiliko ya Katiba yanayohitajika kwa uwekaji wa mkoa (region); pia ilithibitishwa. Baadhi ya maswali ya usawa yanayotokana na maamuzi haya ni:

Ni nani atakayenufaika na sheria hii na kwa njia gani?

Ni nani atapata madaraka (mamlaka, ufikiaji, ufadhili ulioongezeka) kutokana na sheria hii?

Ni nani atapoteza madaraka (mamlaka, ufikiaji, kupunguza ufadhili) kutokana na sheria hii?

Asubuhi ya Alhamisi mapema mliona matokeo ya uteuzi na uchaguzi wa maafisa kwa kamati za kisheria:

Mwanamuke wa Asia – 4 Mwanaume wa Asia – 3 Mwanamuke Mweusi - 10 Mwanaume wa Mweusi – 14 Mwanamuke wa Hispanic/Latina - 2 Mwanaume – 2 Wenye rangi mingi – 4 Mwanaume wa rangi mingi – 1 Mwanamuke wa Pacific Islander - 1 Mwanamuke Mweupe – 17 Mwanaume wa Mweupe – 11 Yasiyo Binary Mweupe - 1

Ingawa asilimia bado inaonyesha idadi kubwa ya maafisa weupe wa Marekani, pia inaonyesha mabadiliko kuelekea “mtandao muhimu wa mahusiano ya mwingiliano” ambao tunauthibitisha katika **Kitabu** chetu cha **Nidhamu**. Katika hamu yetu ya usawa taasisi, tulijiuliza swali lifuatalo: Wakati wa uteuzi, Je, Mchakato, Nafasi, na Utambulisho wa wanachama wa kamati uliongeza au kuzuia uchaguzi, ushiriki, na/au ujenzi wa mahusiano? Mtazamo wa usawa unatualika pia kufikilia athari gani uchaguzi huu unaweza kuwa kwa makundi maalum ya Kanisa la Methodisti Ulimwengu kote.

Kwasabubu ya kihistoria ya ubaguzi ya rangi ya watu, baadhi ya makundi hayatambui wazi mbalimbali kamili ya mataifa yanayowakilishwa kati ya wawakilishi walioteuliwa. Takwimu zilizoripotiwa kwa awali hazikuwa za kutosha kuwakilisha wajumbe 21 kutoka kwa mikutano kuu, 18 kutoka mikutano ya Kiafrika na 3 kutoka mikutano ya Ufilipino, walioteuliwa kama maafisa wakuu au viongozi wa kamati ndogo. Kamati moja tu haikumchagua mtu kutoka kwa mkutano kuu. Baadhi ya mada zilizojitokeza kutokana na ripoti za ufuatiliaji wa mchakato:

- Baadhi ya waangalizi walitambuliwa na kuletwa mbele; wengine walitambuliwa

lakini hawakutajwa majina yao.
- Utambulizi wa wanachama wa kamati kujitambulisha kwa kila mmoja kwa wenzao yalitolewa kwa inayostahiki na baadhi ya maaskofu wakuu; baadhi ya utambulisho ulifanyika baada ya kusisitizwa na mwanachama wa kamati.
- Watafsiri walionekana kuwepo mara nyingi zaidi, ingawa hali moja ilihitaji kusimamisha mchakato mpaka mmoja afike.

Hatimaye, wasiwasi inaendelea kuhusu ibada inaelezwa kila siku. Hii haielekei kwa wasanii wenye vipaji ambao wanatoa fursa nzuri za kati katika Mkutano Mkuu. Katika kile kinachoitwa kama wakati muhimu katika harakati yetu kuelekea Kanisa la Methodist la Ulimwengu kote lenye usawa zaidi na lenye nguvu zaidi, sehemu kubwa ya ibada zimekuwa kwa Kiingereza zikitolewa na washiriki kutoka Marekani. Vipi mambo yangekuwa tofauti ikiwa liturujia zingekuwa kwenye skrini kwa lugha zote rasmi kwenye skrini? Na ikiwa viongozi wa ibada, uteuzi wa muziki, na wasanii wangerejelewa mahusiano ya mwingiliano wa kimataifa tunayoyathibitisha? Tunaposonga mbele, Mkutano Mkuu wetu utahitaji kutilia maanani ni nani anayekaa mezani katika mipango na maamuzi.

# Ripoti ya Ufuatiliaji ya GCSROW Aprili 26, 2024

## Alhamisi, Aprili 25, 2024

Siku ilianza na idadi kubwa ya washiriki katika Mkutano wakiwa wamevalia mavazi meusi tulipoungana na watu kote ulimwenguni kutambua mpango wa Alhamisi wa Baraza la Makanisa Ulimwenguni katika Weusi ambao unafanya kazi kuelekea ulimwengu usio na ubakaji na vurugu. Haja ya Kanisa kutonyamaza tena juu ya suala hili muhimu ililetwa nyumbani kwa njia ya nguvu na Askofu LaTrelle Easterling alipokuwa akihubiri kutoka kwa mtazamo wa uzoefu wake mwenyewe. Hakika tumeitwa kutoka katika ukimya wetu.


Mkutano wa asubuhi ulipoanza, tulimkaribisha Askofu David M. Wilson kuongoza na kusherehekea uwepo wake kama mwenyekiti wa kwanza wa asili wa Marekani kwa kikao cha Konferensi Kuu. Alituita tuagize na akatoa sala katika lugha yake ya asili. Tuliendelea na sherehe huku Askofu Tracy Smith Malone, ambaye atakuwa mwanamke wa kwanza Mweusi kuwa rais wa Baraza la Maaskofu, aliongoza sehemu ya pili ya asubuhi. Ilikuwa asubuhi ya kihistoria.


Wakati wa kikao hicho, 56% ya wawasilishaji kutoka jukwaani walitambuliwa kuwa wanawake na 44% walitambuliwa kuwa wanaume. Katika kikao hiki, 59% ya wasemaji kutoka sakafu walitambuliwa kama wanaume, 34% walitambuliwa kama wanawake na 7% walitambuliwa kama wasio na binary.

Kamati za wabunge zilikutana baada ya chakula cha mchana. Ripoti kutoka kwa kamati mbalimbali zinaonyesha kwamba baadhi ya bikwazo kutoka siku ya kwanza ya mikutano ya shirika imekuwa kushinda na kwamba sisi ni kusonga mbele kwa mfano wa karibu wa mikutano takatifu.

Bado tuna kazi ya kufanya, hasa kamati ndogo zinapokutana. Ni katika hali haya ambapo inaendelea kuwa muhimu kujitambulisha kwa uwazi kabla ya kuzungumza na kuwa wangalifu hasa kuhusu kutosema juu ya mtu mwingine. Ni muhimu pia kwamba kila mtu katika chumba hicho atambue ni nani asiyesikika sauti zake na ni nini kinachozuia sauti hizo kusikika.

Tunapoingia katika siku hii mpya, hebu tujitoe sisi wenyewe na sisi kwa sisi kuwa wawakilishi bora wa upendo wa ajabu wa Mungu na neema.



*Ufunguo: BF - (Mwanamke Mweusi); BM - (Mwanaume Mweusi); H/LF - (Mhispania/Latina Mwanamke); H/LM - (Mhispania/Latino Mwanaume); NAM - (Mwanaume Asili wa Amerika); PIF - (Kike cha Kisiwa cha Pasifiki); WF - (Mwanamke Mweupe); WM - (Mwanaume Mweupe); WNB - (Mweupe wasio binary); MRF - (Wanawake wa rangi nyingi)*

# Maombi Mapya

## Mpango wa Mipangilio wa Sheria za Utaratibu za Conférence Générale

### UTANGULIZI

Kuanzia siku za John Wesley, “Watu waitwao Bamethodiste” bamekusanyika na banaendelea kukusanyika kwa ajili ya kukutana kwa Kikristo kama mbinu za neema. Bamethodiste wa kale, hata baliposhughulikia mahitaji ya kimatendo ya vuguvugu, kimsingi waliangazia masuala ya kiroho. Masuala ya kiroho ya Kanisa na misheni yake kila wakati iko mbele ya mwili iwe ni dhahiri au la katika shauku za mjadala kuhusu wasiwasi za kawaida. Kupitia kukongamana kwa Kikristo Kanisa linakuja pamoja, likitafuta umoja miongoni mwa utofauti, na kila wakati likitamani kujua mawazo ya Kristo. Conférence Générale ndicho chombo wakilishi na zingativu la Kanisa la Methodiste Unie. Limeunda mchakato wenye utaratibu, mantiki na wa haki wa kufanya maamuzi ya wengi katika masuala ya kimatendo ya Kanisa; na bado, pia linalinda haki za misimamo ya wachache. Wawakilshi wanakuja pamoja katika imani kuu kwamba umoja wa Umethodiste Unie ni mapenzi ya Mungu na njia bora zaidi ya “kueneza utakatifu wa kimaandiko” katika vuguvugu hili la kiulimwenguni la Kanisa.

Dhumuni la Mpango wa Mipangilio na Sheria za Utaratibu ni kusaidia Conférence Générale kuwa mbinu za neema, kutambua mapenzi ya Mungu na kutafuta hekima kama ya Kristo katika maamuzi yetu yote. Katikati mwa kutafakatri, tunaweza kusita, kusikiliza kwa kimya, kuomba pamoja, na kuzingatia tena maono yetu kuhusu kule ambapo Roho Mtakatifu analiongoza Kanisa. Nyakati hizi za kimya, maombi na utambuzi zinaweza kuwa tofauti na za kushangaza. Ingawa sio mbadala kwa mjadala wa heshima na wenye utaratibu, zinahudumu kushikilia masuala yetu ya kawaida juu kwa mwangaza wa misheni moja na kubwa zaidi ya Kanisa la Methodiste Unie ili kutengeneza wafuasi wa Yesu Kristo kwa ubadilishaji ulimwengu. Tukiamini kwamba Mungu yuko kazini kote katika maisha yote, Conférence Générale linalialika Kanisa na wengine kuweza kufuatilia tafakari zetu kwa kufanya biashara yetu katika mikutano wazi (kulingana na ¶ 722 ya *Kitabu kya Adabu*).

## MPANGO WA MIPANGILIO

### I. Kikao cha Kufungua na Mipangilio

Mukutano Mkuu utafanyika wakati uliopangwa katika saa na mahali kulikopangwa na kuanza na uabudu. Kikao cha kufungua biashara za Conférence kitaitwa katika utaratibu na askofu mteule, kama ilivyoelezewa katika *Kitabu kya Adabu* ¶16.11.

Utaratibu ufuatao wa biashara utazingatiwa:

A.Orodha ya Usajili. Rekodi ya uhudhurio itatolewa kwa maandishi kwake Secrétaire wa Conférence Générale na:

1) Secrétaire wa Conseil ya Maaskofu kwa niaba ya maaskofu,
2) Secrétaire wa Conseil ya Mahakama kwa niaba ya shirika hilo,
3) Secrétaire Exécutif wa Meza ya Uunganisho kwa niaba ya secrétaire générale,
4) Mwenyekiti wa uwakilishi wa kila conférence ya kimwaka kwa niaba ya ushirika wake (Ona Sheria ya 5), na
5) Mwenyekiti wa kila uwakilishi kwa niaba ya Makubaliano, Makanisa Huru Husika ya Methodiste na Muungano wa Makanisa.

B. Kubainisha waamuzi wa conférence.

C. Ripoti ya Tume ya Conférence Générale.

1) Kukubaliwa na Kutumiwa kwa Mpango wa Mipangilio na Sheria za Utaratibu

D. Uchaguzi

1) Kalenda (Tazama IV.C)

E. Ripoti ya Comité ya Ajenda.

F. Biashara Nyingine.

G. Uahirishwaji.

### II. Hotuba za Maaskofu, Washirika na Watu Wachanga

Hotuba za Kipindi cha Miaka Minne zitatolewa mapema katika Conférence, kwenye saa na wakati utakaoamuliwa na Tume ya Conférence Générale. Conseil ya Maaskofu itaratibu utayarisho na wasilisho la Hotuba ya Maaskofu ya Kipindi cha Miaka Minne. Shirika la Viongozi Washirika wa Conférence ya Kimwaka litaratibu utayarisho na wasilisho la Hotuba ya Washirika ya Kipindi cha Miaka Minne. Fursa hii itakuwa wazi kwa viongozi wote washirika wote wa conférence

ya kimwaka. Kitengo cha Huduma na Watu Wachanga cha Methodiste Unie kitaratibu utayarisho na wasilisho la Hotuba ya Watu Wachanga ya Kipindi cha Miaka Minne. Fursa hii itakuwa wazi kwa watu wote wachanga.

## III. Maafisa Wasimamizi

Maafisa wasimamizi wa majumba ya mijadala ya Conférence, huku jumba la mjadala wa kufungua likiwa halijumuishwi (Tazama Sehemu ya I), watachaguliwa kutoka miongoni mwa maaskofu amilifu na Comité ya Maafisa Wasimamizi (Tazama Sehemu ya VII.A.6).

## IV. Secrétaire wa Conférence Générale

A. Secrétaire wa Conférence Générale atawajibika kwa majukumu yote ya ofisi iliyotolewa na ¶ 504.3 katika matayarisho kikao cha Conférence Générale, na atawajibika kwa Tume ya Conférence Générale.

B. Secrétaire wa Conférence Générale atachagua watu kutoka kwa ushirika wa wachungaji na washirika wa Kanisa la Methodiste Unie ili kuhudumu kwenye vyeo vya wafanyikazi wasaidizi katika ukatibu.

C. Conférence itachamgua Mratibu Kalenda, baada ya kuteuliwa na Secrétaire wa Conférence Générale, ambaye atasaidia Comité ya Ajenda na Kalenda katika kuwasilisha ripoti kwa utaratibu huo ambao utasaidia katika kuharakisha biashara za Conférence, na katika majukumu mengine ya comité (Tazama I.D.1 na VII.A.1).

D. Secrétaire wa Conférence Générale atateua Secrétaire wa Malalamiko ambaye atatayarisha malalamiko, suluhu, na ripoti ambazo zinatimiza mahitajiko ya *Kitabu kya Adabu* ¶ 507 kwa marejeleo kwa comité mwafaka ya sheria, ya kupitiwa na comité ya Marejeleo (Tazama Sehemu ya VII.A.7.).

E. Bajeti ya kazi ya Secrétaire wa Conférence Générale itawasilishwa na Comité ya Conférence Générale kwa Conseil Générale ya Fedha na

Utawala. Bajeti kama hiyo italipiwa kwa Hazina ya Utawala Générale.

F. Kama katika mpito wa vikao vya kipindi cha miaka minne vya Conférence Générale, ofisi ya Secrétaire wa Conférence Générale itapoteza mchapakazi wake kwa sababu yoyote ile, Conseil ya Maaskofu litamteua mrithi wake ili kuhudumu mpaka wakati wa kikao kijacho.

## V. Uteuzi na Uchaguzi

Secrétaire wa Conférence Générale atаunda ratiba ya uwasilishaji uteuzi, uchaguzi wa Conseil ya Maaskofu. Katika kufanya uteuzi na uchaguzi huu, makini itakuwa katika kuhakikisha uendelevu wa ushirika kutoka kipindi kilichopita cha miaka minne. Itakuwa wajibu wa Conseil ya Maaskofu kuwasilisha uteuzi kwa Comité ya Conférence Générale, Comité ya Kudumu ya Masuala ya Conférence Centrale, Comité za utawala za Conférence Générale, na secrétaire mteule wa Conférence Générale. Uteuzi huu utawasilishwa kwa Conférence Générale kwa uchaguzi.

Misimamo ya kinidhamu itatawala taratibu za uteuzi na uchaguzi za:

Conseil Générale ya Fedha na Utawala (¶ 805.1)
Bodi Kuu ya Pensheni na Manufaa ya Afya (¶ 1502.1)
Tume Générale ya Kumbukumbu na Historia (¶ 1704.2)
Seneti ya Chuo Kikuu (¶ 1414.2)
Conseil ya Mahakama (¶¶ 2602, 2603, 2604.1)

na Ushirika wa Maaskofu kwenye:

Conseil Générale ya Kanisa na Jamii (¶ 705.4d)
Conseil Générale ya Bufuatiliaji (¶ 705.4d)
Bodi Générale ya Huduma za Ulimwengu (¶¶ 705.4d, 1311.6)
Bodi Générale ya Elimu ya Juu na Huduma (¶ 705.4d)

*Daily Christian Advocate* itachapisha orodha ya wateule kwa uchaguzi katika Conseil ya Mahakama na Seneti ya Chuo Kikuu. Michoro ya historia ya maisha isiyozidi maneno 100 kwa urefu itawasilishwa na kila mteule na kuchapishwa kama ilivyowasilishwa.

## VI. Tume juu ya Conférence Générale

A.Kutakuwa na Tume ya Conférence Générale itakayojumuisha ushirika wa washirika na wachungaji kama ilivyobainishwa na ¶ 511 ya *Kitabu kya Adabu*. Watakuwa na jukumu la usimamizi kwa mipango yote muhimu kwamkutano wa Conférence Générale.

1. Lugha za Conférence Générale: *Daily Christian Advocate* itachapishwa kwa Kiingereza.[1] Ukalimani wa papo hapo/au wa moja kwa moja wa vikao vya mjadala na vya comité ya sheria utafanywa kwa Kifaransa, Kireno, Kihispania, Kiswahili, Kijerumani, Kirusi, Kikorea, na Lugha ya Ishara ya Kimarekani na/au lugha nyingine kama itakavyoamuliwa na Tume ya Conférence Générale kwa ushauriano na Rasilimali za Lugha Mbalimbali za Bodi Kuu ya Huduma za Ulimwengu.

2. Wakalimani waliothibitishwa kikamilifu au wasaidizi wengine wa kibinafsi kwa watu walio na mahitaji maalum wanaweza kuketi kila inapohitajika pamoja na wawakilishi wanaopiga kura katika vikao vyote vya comité na mjadala.

## VII. Comité

Conférence Générale litakuwa na comité za kudumu na comité maalum kulingana na utaratibu uliopo, zenye majukumu, wajibu na vikwazo fulani kama itakavyopangwa.

### A. Comité za Utawala

Wanachama wa comité zifuatazo watateuliwa na Conseil ya Maaskofu katika mkutano wake wa majira ya vuli unaotangulia Conférence Générale. Wote

[1] Maoni ya mhariri: *Kitabu kya Adhabu 2016* ¶ 511.4.c inahitaji kwamba horaire ya kila siku, ma liste ya maombi, habari za uteuzi, na habari zengine za muhimu sana katika *DCA* inapashwa pia kupatikana kwa Kifaransa, Kiportugais na Kiswahili. Hizi zitatolewa kwa njia ya électronique.

isipokuwa Comité ya Husiano na Marekebisho ya Machapisho watatoka kwenye wawakilishi waliochaguliwa wa Conférence Générale (Tazama Sehemu ya V). Wanachama wa comité za utawala wanaokutana kabla ya siku ambayo Conférence Générale linakongamana watapokea mwakilishi wa kila siku kwa kila siku ya ziada ambayo uhudhurio wao unahitajika. Wawakilishi wanaoteuliwa kwenye comité kama hizo chini ya siku 60 kabla ya kikao cha kufungua cha Conférence Générale watakuwa na haki ya kufidiwa gharama zozote za ziada za usafiri.

*1) Ajenda na Kalenda*

(a) Kutakuwa na Comité ya Ajenda na Kalenda inayojumuisha wanachama kumi na watano, mmoja kutoka kila conférence centrale na mamlaka, angalau sita kati yao watakuwa washirika; Mratibu wa Kalenda; Mwenyekiti wa Comité ya Mipango ya Tume ya Conférence Générale au mteule; na Mwenyekiti wa Tume ya Conférence Générale au mteule.

Hakuna mwanachama wa comité atakuwa mwenyekiti wa comité ya sheria au mfanyikazi wa shirika lolote jumla. Comité itakusanywa, kwa dhumuni la mpangilio, na Secrétaire wa Conférence Générale, au mteule, angalau siku iliyo kabla ya kufunguliwa kwa Conférence Générale. Kufuatia wasilisho na kukubaliwa na kutumiwa kwa ripoti ya Tume ya Conférence Générale katika kikao cha kufungua Conférence Générale, Comité ya Ajenda na Kalenda maramoja itakuwa na wajibu wa kuongoza utaratibu wa biashara wa Conférence.

(b) Comité ya Ajenda na Kalenda ita:

(1) Itawasilisha ripoti za kalenda katika utaratibu ambao utaharakisha biashara za Conférence,

(2) Itamfahamisha askofu msimamizi punde iwezekanavyo kuhusu vipengee vya ajenda, ukijumuisha utaratibu wa upaumbele, wa kuzingatiwa,

(3) Itahifadhi muhtasari wa maendeleo ya kalenda;

(4) Mapendekezo ya ripoti kwa kila kikao cha Conférence Générale kuhusiana na ajenda ya biashara, ikijumuisha ugavi wa muda na utaratibu ambao ripoti ya comité za sheria zitawasilishwa;

(5) Itapeana upaumbele katika mjadala kwa uzingatiaji wa sheria jinsi vipengee vya kalenda vinavyopatikana: kwa vipengee vinavyoathiri kanisa la ulimwenguni, kwa vipengee vyenye athari ya kifedha, vipengee vinavyoungewa mkono na comité ya sheria, na vipengee venye ripoti za wachache;

(6) Itatangaza ajenda inayotazamiwa kufuatwa kwenye siku inayofuata, katika kikao cha mwisho cha mjadala cha kila siku;

(7) Itashauriana kila siku na wenyekiti wa comité ya sheria ili kutekeleza biashara ya Conférence Générale; na

(8) Itapokea maombi yote ya taratibu maalum za siku, isipokuwa tu zile ziko kwenye ripoti ya Tume ya Conférence Générale kwenye siku ya kwanza ya Conférence.

(c) Mapendekezo, maswali, mawasiliano, suluhu, na masuala mengine ambayo hayajajumuishwa katika biashara ya kawaida ya Conférence Générale yatatumwa kwa Comité ya Ajenda na Kalenda bila azimio au mjadala. Comité hii itaamua kana kwamba suala lililowasilishwa litazingatiwa na Conférence Générale. Uamuzi wa comité hii unaweza kukatiwa rufaa kwa kuwasilisha saini za wawakilishi kumi kwa Conférence. Kipengee hicho kitawasilishwa kwa Conférence ikiwa rufaa inaungwa mkono kwa kura thuluthi moja.

*2) Husiano na Marekebisho ya Machapisho*

Kutakuwa na Comité ya Husiano na Marekebisho ya Machapisho ya watu wanne watu wanane na wengine wawili mbadala ambao sio wawakilishi katika Conférence Générale, na Mhariri wa Kitabu au mteule, ambaye atakuwa mshirika rasmi wa zamani. Watakuwa na haki ya kufidiwa gharama za uhudhurio katika mikutano ya comité. Mhariri wa Kitabu au mteule ataikusanya comité kwa dhumuni la mpangilio. Wakati wa kikao cha Conférence Générale na kufuatia kuahirishwa kwake, jukumuJukumu la comité hii litakuwa:

(a) Kupitia sheria zote zilizopendekezwa na kuripotiwa katika *Daily Christian Advocate* au kuwasilishwa kwa Conférence Générale katika ripoti maalum. Comité itaripoti kwa comité husika, au kwa Conférence Générale kulingana na vile hali itakavyohitaji, mikinzano yote, unakili wote, na kasoro zote zinazogunduliwa.

(b) Kuhakikisha kwamba, wakati kipengee cha kalenda kilichoidhinishwa kwenye Kalenda ya Ridhaa au chini ya kura jumuishi kinapatikana kuwa kinabishana na sehemu nyingine ya kipengee cha kalenda kilichojadiliwa na kupigiwa kura katika kikao cha mjadala, basi kipengee hicho kilichojadiliwa na kupigiwa kura kitaibuka mshindi.

(c) Éditer *Kitabu kya Adhabu* kulingana na Sehemu ya X.B.

*3) Hisani na Fadhila*

Kutakuwa na Comité ya Hisani na Fadhila itakayojumuisha wanachama kumi na wawili, mmoja kutoka kila conférence centrale na mamlaka, angalau sita kati yao watakuwa washirika. Comité itakusanywa na askofu kwa dhumuni la mpangilio. Comité hiyo inayo majukumu na wajibu zifuatazo:

(a) Kuzingatia masuala yote ya fadhila na, inavyofaa, kupendekeza kwa Conférence yasikilizwe.

(b) Kuzingatia suluhu za mapendekezo, hisani, shukrani, n.k., yaliyowasilishwa na wawakilishi kwa maandishi. Comité inaweza kuanzisha suluhu kama hizo na inaweza kuhariri na kurekebisha zile zilizowasilishwa kwake. Suluhu zilizoidhinishwa na comité zitachapishwa kwenye *Daily Christian Advocate* na kuletwa kwenye jukwaa comité ikizizingatia kuwa zenye umuhimu au dharura isiyokuwa ya kawaida.

(c) Kufanya mipango ya kupanua mahakama zenye zinafaa za Mkutano.

(d) Kuwekea ripoti yake mipaka kwa muda usiopita dakika kumi katika siku yoyote moja ya biashara, ikijumuisha kauli ya mwenyekiti na kesi za watu hao kama inavyoweza kuwasilishwa. Hakuna mtu wala watu watawasilishwa ambao ombi lao limekataliwa na Tume ya Conférence Générale, wala baada ya siku ya

sita isipokuwa tu kama imeidhinishwa na kura thuluthi mbili za Conférence (Tazama Sheria ya 31.6).

*4) Stakabadhi*

Kutakuwa na Comité ya Stakabadhi itakayojumuisha wanachama kumi na wawili, mmoja kutoka kila conférence centrale na mamlaka, angalau sita kati yao watakuwa washirika. Comité itakusanywa na askofu kwa dhumuni la mpangilio. Comité hiyo itatoa mwongozo kwa Secrétaire wa Conférence Générale kuhusiana na kuidhinishwa kwa stakabadhi za wawakilishi, na inaweza kupitia maamuzi kuhusiana na kuketi kwa wawakilishi, ikijumuisha wawakilishi wa akiba. Comité itaripoti kwa Conférence Générale maamuzi na mapendekezo yake kuhusiana na changamoto za kuketi kwa wawakilishi wowote.

*5) Jarida*

Kutakuwa na Comité ya Jarida ya wawakilishi watatu ya kuidhinisha kila siku rekodi ya maendeleo ya Conférence Générale zilizotayarishwa na Secrétaire wa Conférence Générale na msaidizi/wasaidizi. Comité itakusanywa na askofu kwa dhumuni la mpangilio.

*6) Maafisa Wasimamizi*

Kutakuwa na Comité ya Maafisa Wasimamizi itakayojumuisha wanachama kumi na wawili, mmoja kutoka kila conférence centrale na mamlaka, sita kati yao watakuwa wachungaji na sita kati yao watakuwa washirika. Comité itakusanywa na askofu kwa dhumuni la mpangilio. Comité itachagua na kufahamisha afisa msimamizi (maafisa wasimamizi) wa kila kikao cha mjadala angalau saa 24 mapema, kadri iwezekanavyo. Comité itakuwa huru kumchagua askofu kwa zaidi ya kikao kimoja na kumbadilisha afisa msimamizi wakati wa kikao, wakati wowote inapokuwa na haja ya kufanya hivyo (Tazama Sehemu ya III).

*7) Marejeleo*

Kutakuwa na Comité ya Marejeleo itakayojumuisha wanachama ishirini na wanne, mchungaji mmoja na mshirika mmoja kutoka kila conférence centrale na mamlaka. Uanachama wa Comité hii utajumuisha angalau mwanachama mmoja kutoka kila comité ya sheria ambaye atateuliwa kama mratibu

malalamiko kwa niaba ya comité yao ya sheria. Ikiwa itawezekana, waratibu malalamiko wanafaa kuwa wamehudumu hapo awali kwenye comité ya sheria ya Conférence Générale. Waratibu malalamiko hawa watahudumu kama washauri kwa maafisa wa comité ya sheria ambayo wao ni wanachama. Wanachama wa ziada kutoka Comité ya Marejeleo watamsaidia mratibu malalamiko katika comité ya sheria ambayo wao ni wanachama. Comité hii itakusanywa, kwa dhumuni la mpangilio, na Secrétaire wa Conférence Générale, au mteule, siku ya kabla ya Conférence Générale kufunguliwa.

(a) Baada ya kupitia kazi zilizopendekezwa na Secrétaire wa Conférence Générale wa malalamiko, suluhu, na mawasiliano sawia yanayoshughulikia biashara ya kawaida ya Conférence kwa comité za sheria, comité hii itatuma masuala yayo hayo kwa comité mwafaka za sheria (Tazama Sehemu ya IV.D). Comité hii itakuwa na jukumu la kupitia kazi, iliyofanywa na Secrétaire wa Conférence Générale, ya ripoti, mapendekezo, na suluhu zote kutoka kwa mashirika jumla, tume na comité za kudumu au maalum, na mawasiliano yote mengine ambayo yanawasilishwa kwa Secrétaire wa Conférence Générale baada ya kukusanyika kwa Conférence Générale, yote ambayo yatatumwa moja kwa moja kwa comité mwafaka za sheria bila ya kuwasilishwa kwa kikao cha mjadala cha Conférence Générale.

(b) Comité ya Marejeleo inaweza kuondoa kipengee ambacho kimepewa comité, aidha baada ya ombi au baada ya azimio lake binafsi. Inaweza pia kusitisha kurejelewa au kuchapishwa kwa waraka wowote ambao itachukulia haifai.

(c) Secrétaire wa Conférence Générale, au Secrétaire wa Malalamiko, anaweza kusitisha kuchapishwa kwa malalamiko yoyote yatakachukuliwa kuwa ni ya kuchafua jina la mtu binafsi au ambayo hayafai kamwe. Comité ya Référence itapitia maamuzi yote kama hayo.

(d) Pale ambapo Comité itapata malalamiko mawili au zaidi ambayo yanafanana kwa kiasi kikubwa, inaweza kuyaweka pamoja katika kichwa na nambari moja, na kuonyesha jumla ya idadi ya malalamiko.

(e) Hakuna malalamiko ambayo yatatolewa na Comité ya Marejeleo kwa comité yoyote ya Conférence Générale isipokuwa yanatimiza mahitajiko ya *Kitabu kya Adabu*.

**B. Kabla ya Kundi ya Utafiti wa Kisheria**

(a) Kumekuwa na Panel ya Utafiti ya Sheria ambayo imechaguliwa na Comité Exécutif ya Tume ya Conférence Générale, ambayo ina mebre sawa na ile ya comité ya sheria.

(b) Membre wa panel batachaguliwa kulingana na ufahamu mwingi wa *Kitabu kya Adabu* kama ilivyoonyeshwa na wao kushiriki hapo mbele katika maisha ya kanisa jumla kupitia huduma kwenye Conseil ya Mahakama, Comité ya Uhusiano na Marekebisho ya Machapisho, au kama chancelier wa conférence. wawe tayari kujitolea saa nyingi kabla ya Conférence Générale.

(c) Maoni yoye yanayopokewa baada ya kuunganishwa na paragraphe za kinidhamu, yatatumwa kwa comité ya sheria katika mebre wa panel. Membre wa panel, na wao batapitia maombi ambayo wamepatiwa na kutafuta paragraphe ingine ya *Kitabu kya Adabu*, pamoja na Katiba ambayo inahusiana na ombi, na pia maamuzi na memoranda ya Conseil ya Mahakama ambayo inahusiana kwa karibu. membre wa panel atarekodi paragraphe, uamuzi au memoranda inayohusiana na kila ombi.

(d) Hakuna uamuzi au maoni ya machapisho kuhusu lalamiko lolote yatajumuishwa.

(e) Paragraphe zinazohusiana zitaambatishwa kabisa na maoni hayo yanapopelekwa kwenye mchakato wa comité ya sheria ya Conférence Générale.

(f) Comité ya sheria itaangalia vile paragraphe zinazohusiana zinavyoathirika na kukubali ombi.

(g) Kazi ya Jopo la Sheria la Utafiti la Awali itaratibiwa na Secrétaire wa Maombi

(h) Mwanachama wa kundi hajazuiliwa kuwa mwakilishi katika Conférence Générale.

**C. Comité ya Maadili**

Kutakuwa na Comité ya Maadili, itakayojumuisha wanachama wa Comité ya Mpango wa Mipangilio na Sheria za Utaratibu wa Conférence Générale. Bajumbe binafsi banaweza kuripoti wasiwasi zao kuhusu ukiukaji uliofanyika kwa Ofisi ya the Secrétaire wa Conférence Générale. Ofisi ya Secrétaire wa Conférence Générale atachunguza, na kujaribu kusuluhisha madai yote, na kuripoti suluhu kwa Comité ya Maadili na kwa bajumbe ambao walitoa wasiwasi hiyo. Kulingana na gravité ya wasiwasi hizo, Ofisi ya the Secrétaire wa Conférence Générale anaweza kutuma suala hilo kwa Comité ya Maadili. Madai ya ukiukaji sheria yanaweza pia kutumwa moja kwa moja kwa Comité ya Maadili kwa humsi moja ya kura za Kikao cha Mjadala. Comité ya Maadili itapitia masuala yote yaliyotumwa kwake na kuripoti matokeo yake kwa Kikao cha Mjadala pamoja na hatua iliyopendekezwa.

**D. Comité ya Kudumu ya Mambo ya Mkutano wa Kati**

(Kwa ushirika, tazama *Kitabu kya Adabu* ¶ 2201.)

Kwa Comité hii kutatumwa malalamiko yote, suluhu zote, n.k. yanayohusiana na Conférence za Kati, Makanisa Huru ya Methodisti, Makanisa Huru Husiani ya Methodisti, Muungano wa Makanisa Husiani na Husiano za Makubaliano.[2]

*Kitabu kya Adabu* ma paragraphe za

28-31………………Katiba: Conférence Centrale
540-548……………Conférence Centrale

[2] Maoni ya mhariri: Maeleoz ya nyenzo za sheria, pamoja na paragraphe zake, yamekuwa update ili kuonyesha nyenzo hiyo ilivyoshughulikiwa na Tume ya Conférence Générale kulingana na ¶ 511.4.f.

560-567……………Conférence Centrale za Muda

572 ………………..Kuwa Mumethodiste Autonome, Mumethodiste Autonome Mshirika, au Kanisa Unie ya Ushirika kutoka Conférence Centrale

575………………...Kujiunga na Kanisa la Methodiste Unie

2201……………….Comité ya Kudumu ya Masuala ya Conférence Centrale

Comité ya Kudumu ya Masuala ya Conférence Centrale itawasilisha ripoti yake na mapendekezo yoyote ya sheria yanayohusiana na aya ambazo imepewa moja kwa moja na Conférence Générale. Ikiwa Comité ya Kudumu ya Masuala ya Conférence Centrale ina wasiwasi na aya zozote zilizopewa mojawapo ya comité za sheria, Comité hiyo itatoa pendekezo lake kwa comité mwafaka ya sheria ili kuzingatiwa na pendekezo kutolewa kwa Conférence Générale.

**E. Comité za Kisheria**

Kutakuwa na comité za sheria ambazo zitapewa malalamiko na ripoti zote zilizowasilishwa vyema. Tume ya Conférence Générale itapanga idadi ya comité za sheria na upeanaji aya na mada za Kinidhamu kwa comité hizo kwa ushauriano na Secrétaire wa Conférence Générale na Meneja wa Biashara wa Conférence Générale (¶ 511.4.f). Comité yoyote ya sheria inayozingatia sheria inayoathiri majukumu yaliyopewa Comité ya Kudumu ya masuala ya Conférence Centrale itashauriana na Comité hiyo kabla ya kuwasilisha pendekezo lake la sheria kwa Conférence.

**F. Uanachama ya Comité za Sheria**

1) Ndani ya uwakilishi wa conférence ya kimwaka, kila mwakilishi atachagua comité moja ya sheria kwa ambayo atahudumu, chaguo likifanywa kulingana na utaratibu wa uchaguzi.

Miaka ya 2020, washirika baliochaguliwa kwanza~~,~~ watakuwa na haki ya chaguo la kwanza, mwakilishi mchungaji aliyechaguliwa kwanza, chaguo la pili, na hivyo basi haki ya chaguo itaendelea kubadilishana kati ya wawakilishi bachungaji na wawakilishi

washirika na bachungaji kwa utaratibu wa uchaguzi wao. Kwa Conférence Générale zinazofuatia, chaguo la kwanza litabadilishana kati ya wawakilishi washirika na wawakilishi wachungaji na washirikakulingana na utaratibu ufuatao:

| | |
|---|---|
| Bashirika | wa mwaka wa 2024 |
| Bachungaji | wa mwaka wa 2028 |
| Bashirika | wa mwaka wa 2032 |
| Bachungaji | wa mwaka wa 2036 |
| Bashirika | wa mwaka wa 2040 |
| Bachungaji | wa mwaka wa 2044 |

Banachama bawili wa uwakilishi hawawezi kuhudumu kwenye comité sawia ya sheria isipokuwa uwakilishi husika umewakilishwa katika pande zote. Wakato wowote ambapo uwakilishi una zaidi ya mwakilishi mmoja kwenye comité ya sheria, wawakilishi wake watagawanywa kwa mgao sawa unaowezekana kati ya washirika na wachungaji. Hivyo basi, ikiwa kuna wawakilishi watatu kwenye comité, kutakuwa na wachungaji wawili na mshirika mmoja au kinyume. Secrétaire wa Conférence Générale atatoa maelekezo haya na mifano hii na maelekezo ya uchaguzi wa wawakilishi kutumwa kwa secrétaire wa kila conférence ya kimwaka.

2) Ikiwa suala lingali linazingatiwa katika comité yoyote ya sheria ambayo katika uamuzi wa uwakilishi wowote wa conférence ya kimwaka unaathiri pakubwa maslahi ya wote wanaohusika, na ikiwa conférence husika ya kimwaka halijawakilishwa katika uanachama wa comité husika, basi uwakilishi unaweza kuchagua mmoja wa wawakilishi wake kuwakilisha conférence yake la kimwaka katika comité wakati suala lililotajwa hapo awali lingali linazingatiwa. Mwakilishi huyu atakuwa na haki ya kuketi na comité wakati suala hili linazingatiwa na atakuwa na uwezo wa kutoa maoni, lakini sio kupiga kura (Tazama Sehemu ya VII.G.3.(e)).

3) Kila mtu aliyeketi katika Conférence Générale mwenye uwezo wa kutoa maoni lakini sio kupiga kura anaweza kuwasilisha kwa Secrétaire wa Conférence Générale chaguo la comité ya sheria na atakuwa na haki sawia katika comité ya kutoa maoni na sio kupiga kura.

**G. Mikutano ya Comité**

1) Mpangilio na Akidi ya Comité. Comité zote za sheria na utawala zitakutana kwa minajili ya mipangilio wakati utakaoamuliwa na Tume ya Conférence Générale. Winge wa wanachama watajumuisha akidi kwa ajili ya kufanya biashara katika comité zote.

Kulingana na roho wa ¶ 722 katika *Kitabu kya Adabu*, mikutano ya Comité na comité ndogo za Conférence Générale itakuwa wazi.

2) Comité za Utawala

(a) Askofu aliyeteuliwa na Conseil ya Maaskofu na secrétaire mpangaji aliyeteuliwa na Secrétaire wa Conférence Générale watahudumu, kama mwenyekiti na secrétaire mtawalia, ili kupanga comité, isipokuwa pale ambapo msimamo mwingine umebainishwa.

(b) Uchaguzi wa mwenyekiti, makamu mwenyekiti na secrétaire wa kila comité ya utawala utafanywa kwa sanduku la kupigia kura lililo kando na lililoandikwa kwa kila cheo. Uzingatiaji kamili utapewa ujumuishaji unaoonyesha hali ya kiulimwengu ya kanisa, ikijumuisha jinsia, umri, kabila, jiografia, watu wachanga, wachungaji, na washirika.

3) Comité za Sheria

Comité zote za sheria zitakutana kwa ajili ya mipangilio wakati ule ambao Tume ya Conférence Générale itaamua. Askofu aliyeteuliwa na Conseil ya Maaskofu na secrétaire mpangaji aliyeteuliwa na Secrétaire wa Conférence Générale watahudumu, mtawalia, kama mwenyekiti na secrétaire, ili kupanga kila moja ya comité hizo kadhaa. Mkutano wa kwanza wa comité za sheria utaandaliwa punde iwezekanavyo kufuatia kikao cha kwanza cha mjadala cha Conférence Générale. Maelezo mbalimbali kwa comité, ikifuatiwa na uchaguzi wa maafisa, ndio utakaokuwa utaratibu wa biashara wa mkutano wa kwanza wa comité.

(a) Uchaguzi wa Maafisa. Mwenyekiti, makamu mwenyekiti, secrétaire, na wenyekiti wa comité ndogo wa kila comité watachaguliwa kwa sanduku la kupigia kura lililoandikwa kwa kila cheo. Uzingatiaji kamili utapewa ujumuishaji

unaoonyesha hali ya kiulimwengu ya kanisa, ikijumuisha jinsia, umri, kabila, jiografia, watu wachanga, wachungaji, na washirika. Ikiwa hakutakuwa na mshindi kwa kura ya wengi kati ya wanaopiga kura baada ya kura kupigwa mara tatu (3) mtawalia, basi jukwaa litakuwa wazi tena kwa uteuzi kufanyika.

(b) Mafunzo. Secrétaire wa Conférence Générale atakuwa na jukumu la kutoa mafunzo kwa wenyekiti, makamu wenyekiti,makatibu, na wenyekiti wote wa comité ndogo za comité za sheria. Mafunzo haya yatajumuisha maelekezo katika majukumu yao, taratibu zote za kushughulikia malalamiko, nyakati za mida ya mwisho ya kila siku ya kuchapisha ripoti, na taarifa nyingine ili kuharakisha kazi ya comité. Tume ya Conférence Générale itapanga saa na mahali pa kikao hicho cha mafunzo. Hakuna afisa atakayehudumu bila kukamilisha mafunzo haya.

(c) Wabunge. Kila comité ya sheria itapewa mbunge na Secrétaire wa Conférence Générale. Maaskofu Waliostaafu walioteuliwa na Conseil ya Maaskofu watajumuishwa katika kundi la wabunge. Itakuwa wajibu wa Meneja wa Biashara wa Conférence Générale kuendeleza kundi la watu wengine ambao wakati huo sio wawakilishi ili wahudumu kama wabunge. Inapendelewa kwamba watu hawa wawe washirika wa Kanisa la Methodiste Unie, wawe na maarifa ya Sheria za Conférence Générale, na wawe na mafunzo ya utaratibu wa bunge. Maaskofu waliostaafu watapewa upaumbele katika kupeanwa kwa comité za sheria. Kwa mwaliko wa afisa msimamizi, mbunge anashauriana kuhusu masuala ya utaratibu wa bunge.

(d) Mikutano ya Mara kwa Mara. Comité za sheria zitakutana kufanya biashara kama ilivyoratibiwa na Comité ya Ajenda na Kalenda isipokuwa iamuliwe vinginevyo na Conférence, na katika nyakati hizo kama vile comité inaweza kuamua mradi tu hakuna comité ya sheria itakutana nyakati zinazokinzana na vikao vya mjadala.

(e) Eneo ya Kupigia Kura. Kila comité ya sheria na comité ndogo itapanga eneo maalum ambalo wanachama wa comité wanaopiga kura na wasaidizi au watafsiri wao wenye idhini mwafaka pekee yao watakuwa wameketi. Meneja

wa Biashara wa Conférence Générale atatoa viti vinne teule katika kila comité ya sheria kwa wafutailiaji wa kutoka kwa Tume Kuu ya Dini na Mbari na Tume Kuu ya Hadhi na Jukumu la Wanawake. Eneo lingine litapangwa pia kwa bale baliopo benye uwezo wa kutoa maoni lakini sio kupiga kura (Tazama Sehemu ya VII.F.2). Wafanyikazi wa Secrétaire wa Conférence Générale na Meneja wa Biashara wa Conférence Générale wanaweza kuongea katika utendakazi wa majukumu yao. Wafanyikazi wa mashirika jumla, wanarasilimali wengine, na wageni wanaweza kuongea tu baada ya kuidhinishwa, kila mara kupitia hatua mahsusi ya kamativkwa kura thuluthi moya za comité au comité ndogo au kwa mwaliko wa mwenyekiti (Tazama Sheria ya 31.3).

(f) Ripoti za Wachache. Ripoti za wachache zinaruhusu uwasilishaji mitazamo inayotofautiana inayoshikiliwa na sehemu kubwa ya comité ya sheria na inaweza kutolewa kulingana na sheria ya 29, 38, na 39.

(g) Ripoti. Ripoti za Comité ya Sheria zinafaa kuwasilishwa punde iwezekanavyo kufuatia hatua ya comité. Ripoti zote za Comité ya Sheria zitawasilishwa kabla ya saa 17h00 siku ya Jumatatu ya wiki ya pili.

**H. Kazi na Mamlaka ya Comité**

1) Comité za utawala, bila elekezo au mwelekeo mahsusi kutoka kwa Conférence, zitakuwa na jukumu la kuzingatia na kuripoti kwa Conférence kuhusu masuala yote yaliyo ndani ya majukumu yao husika (Tazama Sehemu ya VII.A).

2) Comité za sheria zitazingatia na kuripoti kuhusu kile ambacho kimetumwa kwao kutoka kwa Comité ya Marejeleo au kile ambacho kimetumwa kwao moja kwa moja na Conférence (Tazama Sheria ya 36).

## VIII. Pendekezo Linalohusu Matumizi ya Fedha Ambazo Hazijawekwa Kwenye Bajeti

A. Hatua yoyote iliyopendekezwa kwa kikao cha mjadala cha Conférence Générale la kuanzisha bodi, tume, comité, au jopokazi la mpito au endelezi, itatumwa kwa Baraza Kuu la Fedha na Utawala na Meza ya Uunganisho au comité zao tendaji au kundi lao la uhakiki wa matumizi ama mapitio ya matumizi kundi lao la upitiaji matumizi ili

kupata ripoti na pendekezo kabla ya hatua ya mwisho kuchukuliwa. Baraza Kuu la Fedha na Utawala na Meza ya Uunganisho au comité zao tendaji au kundi lao la upitiaji matumizi litapatia Conférence Générale yafuatayo kabla ya hatua kuchukuliwa:

1) bajeti iliyokadiriwa ya bodi, tume, comité au jopokazi lililopendekezwa kwa kipindi cha miaka minne ijayo; na

2) kauli inayoelezea jinsi uundaji wa bodi, tume, comité, au jopokazi lililopendekezwa utakavyoathiri bajeti ya au za bodi, tume, comité na majopokazi yaliyopo ambayo tayari yamewasilishwa na Baraza Kuu la Fedha na Utawala.

B. Hatua yoyote iliyopendekezwa kwa kikao cha mjadala cha Conférence Générale ambayo inahusisha matumizi ya fedha itatumwa kwa Baraza Kuu la Fedha na Utawala na Meza ya Uunganisho au comité zao tendaji au kundi lao la upitiaji matumizi ili kupata ushauri na pendekezo kabla ya hatua ya mwisho kuchukuliwa. Maombi yoyote ya mashirika jumla ya fedha za ziada yatatambuliwa hivyo; vinginevyo, yatazingatiwa kuwa yamejumuishwa ndani ya bajeti ya shirika.

C. Pendekezo lolote lililochini ya misimamo ya sehemu hii litapendekezwa kwa Baraza Kuu la Fedha na Utawala na Meza ya Uunganisho au Comité zao tendaji au kundi lao la upitiaji matumizi angalau saa sabini na mbili kabla ya uahirishwaji ulioratibiwa wa Conférence Générale.

## IX. Gharama ya Bawakilishi

A. Gharama kamili za usafiri na za kila siku zitalipwa kwa idadi ya wawakilishi wa kupiga kura kutoka kila Conférence kulingana na ripoti ya mwenyekiti wa kila uwakilishi wa conférence ya kimwaka. Ikiwa wakati wa conférence, mwakilishi wa hifadhi ameketi kwa niaba ya mwakilishi mkuu kwa siku moja nzima au zaidi, mwakilishi mkuu atebadilisha gharama za kila siku kulingana na mwakilishi huyo wa hifadhi kimsingi na muda uliohudumiwa na kila mmoja.

B. Usafiri wa ndege utakuwa kwa nauli ya kiuchumi zaidi ya kuenda na kurudi moja kwa moja kuelekea na kutoka kwenye eneo la Conférence Générale. Nauli za safari maalum na ukuzaji zitatumiwa wakati wowote iwezekanavyo. Gharama za ziada zinaweza kuruhusiwa kwa wawakilishi kutoka conférence iliyo nje ya Marekani ili waweze kufika na kuondoka kwa kipindi kisichozidi siku mbili kabla au baada ya Conférence Générale. Marupurupu ya gharama za kila siku za siku hizo kabla na baada ya Conférence Générale yatakuwa katika kiwango sawia na yanayoruhusiwa wawakilishi wakati wa Conférence Générale. Ubaguzi kwa vikwazo hivi ni lazima uidhinishwe na Meneja wa Biashara wa Conférence Générale.

C. Wakati mwakilishi mmoja au zaidi wanapokuja kwa gari moja, mmiliki wa gari hilo atafidiwa gharama halisi ya usafiri (maegesho, umbali uliosafiriwa na ada alizolipia, milo na malazi njiani). Umbali uliosafiriwa utafidiwa kwa kiwango cha biashara kilichofikiwa na IRS na utapimwa kuanzia mahali pa kutoka hadi eneo la Conférence Générale na kurudi. Milo na malazi zitafidiwa hadi kufikia kiwango kilichowekwa cha pesa za kila siku za conférence générale. Wakati safari ya kuenda na kurudi inapozidi maili 1,000 kwa safari yoyote ile ya kuenda na kurudi, gharama ya usafiri italipwa aidha kulingana na gharama halisi kama ilivyobainishwa hapo juu au kwa nauli ya ndege ya kiuchumi zaidi inayopatikana pamoja na gharama zozote za usafiri zinazohusiana uwanjani mwa ndege, yoyote ile ambayo iko chini zaidi. Abiria ambao ndio wawakilishi wakuu wa kupiga kura kwenye Conférence Générale watawasilisha tu gharama ya chumba na milo njiani hadi kufikia kiwango kilichowekwa cha kila siku cha Conférence Générale.

D. Kwa tarehe ambazo Conférence Générale lina vikao, hakuna mwakilishi wa Conférence Généraleu atapokea pesa za gharama kutoka kwa Kanisa jumla au yoyote ya bodi na mashirika yake isipokuwa kiwango cha kila siku na gharama za usafiri zilizoidhinishwa zinazopatikana kwa wawakilishi. Msimamo huu si wa kuwekea vikwazo usaidizi rasmi kwa wawakilishi kutoka conférence zao binafsi za kimwaka.

### X. Nyenzo za Kujumuishwa katika *Kitabu kya Adabu*

A. Nyenzo zisizo za sheria (Kurasa za 1- 24, 2016 *Kitabu kya Adabu*) zitatumwa kwa Comité ya Husiano na Marekebisho ya Machapisho ili kuzingatiwa na ushauriano uwezekanao na Tume Kuu ya Kumbukumbu na Historia au kutumwa kwa Comité ya Marejeleo.

B. Mhariri wa Kitabu, Secrétaire wa Conférence Générale, Mchapishaji wa Kanisa la Methodiste Unie, na Comité ya Uhusiano na Marekebisho ya Machapisho watapewa jukumu la kuhariri *Kitabu kya Adabu*. Marekebisho yoyote ya Kinidhamu ambayo hayategemei marekebisho ya katiba ili kuanza kutumika yatajumuishwa katika aya mwafaka za *Kitabu kya Adabu* kwa utaratibu wa kukubaliwa na kuanza kutumiwa kwa marekebisho hayo.

Wahariri, katika utekelezaji uamuzi wao, watakuwa na mamlaka ya kufanya mabadiliko kwa maneno kama inavyohitajika ili kupatanisha sheria bila kubadilisha maudhui yake. Wahariri, kwa ushauriano na Conseil ya Mahakama, pia watakuwa na mamlaka ya kufuta misimamo yoyote ya *Kitabu kya Adabu* ambayo imeamuliwa kinyume na katiba na Conseil ya Mahakama. Pingamizi yoyote dhidi ya uamuzi uliofanywa na Comité ya Husiano na Marekebisho ya Machapisho itakuwa kwa maandishi. Suala hilo likifikia Conseil ya Mahakama, mhusika anayekata rufaa atatoa ilani hapo baadaye kwa Comité. Hitilafu yoyote inayopatikana katika maandishi ya *Kitabu kya Adabu* itatumwa na Jumba la Uchapishaji la Methodiste Unie kwa Conseil ya Maaskofu, Secrétaire wa Conférence Générale, Secrétaire wa Conférence za Kimwaka, na Wakurugenzi wa Conférence za Kimwaka wa Huduma za Uunganisho, na itachapishwa na Mhariri wa Kitabu kwenye tovuti ya Jumba la Uchapishaji la Methodiste Unie.

Marekebisho ya katiba yaliyoidhinishwa kulingana na ¶ 59 na sheria inayowezesha iliyokubaliwa na kuanza kutumiwa katika tarajio la marekebisho ya Katiba yatachapishwa na mhariri wa Kitabu kwenye tovuti ya Jumba la Uchapishaji la Methodiste Unie kufuatia kuidhinishwa. Yatachapishwa kwenye *Kitabu kya Adabu* kinachofuatia. Marekebisho ya katiba yataanza kutumika wakati wa kuidhinishwa. Sheria inayowezesha itaanza kutumika mnamo Januari 1, ya mwaka unaofuatia kuidhinishwa kwa marekebisho ya katiba na itaanza kufanya kazi ni kana kwamba ilikuwa imeanza kutumika baada ya mabadiliko mengine yote ya kinidhamu yanayoathiri paragraphe fulani.

### XI. Usambazaji Nyenzo miongoni mwa Waamuzi wa Conférence

Baada ya siku ya kwanza, *Daily Christian Advocate*, ~~na~~ nyenzo zinazohusu wasilisho za Conférence Générale na kuzalishwa na mashirika rasmi ya Kanisa la Methodiste Unie, na marekebisho yanayopokewa vizuri, ikiwa

yataidhinishwa na Secrétaire wa Conférence Générale, zitasambazwa kwa njia ya kurasa. Kurasa hizi zitasambaza mawasiliano kwa wawakilishi binafsi mradi tu mawasiliano hayo yawe na jina na eneo la mpokeaji na mtumaji.

**XII. Usambazaji Nyenzo Nje ya Jumba la Mjadala au Chumba cha Comité**

Majarida au nyenzo zozote maalum kutoka kwa bodi na mashirika ya Methodiste Unie, pamoja na makundi husika ya Methodiste Unie zinaweza kusambazwa chini ya masharti yafuatayo:

A. Nakala moja ya kila kipengee itawasilishwa kwa ofisi ya Tume ya Conférence Générale kabla ya usambazaji.

B. Nyenzo zilizosambazwa zitakuwa zinahusu Conférence Générale na wala sio za kutafuta uanachama katika shirika lolote.

C. Hakuna msambazaji atakayeruhusiwa kusambaza ndani ya kituo cha mkutano isipokuwa kama amepata idhini kwa maandishi kutoka kwa Meneja wa Biashara wa Conférence Générale. Kila kundi litakuwa na mwasiliani mmoja atakayesajili wanachama wote wa kundi na kupokea utambulisho wa kila mwanachama.

D. Usambazaji utakuwa angalau futi 30 nje ya mlango wowote wa kiingilio kwenye kikao cha mjadala au kwenye chumba cha comité.

E. Usambazaji utafanywa na wawakilishi wa makundi yaliyotajwa hapo juu. Ni jukumu la wasambazaji kutoingilia au kuhitilafiana na kiingilio au kitokeo cha watu au kuzuia mkondo wa kawaida wa watu wanaotembea.

F. Basambazaji bana jukumu la kutupa nyenzo zozote ambazo hazijatumika au hazijachukuliwa na benyewe.

G. Basambazaji banaokiuka kanuni hizi batapigwa marufuku ya kusambaza nyenzo siku za usoni.

## XIII. Ripoti Zisambazwe Kabla ya Conférence Générale

Ripoti, mapendekezo, na suluhu zinazohitaji hatua ya Conférence Générale, pamoja na malalamiko yaliyowasilishwa kulingana na *Kitabu kya Adabu* ¶ 507.7, kwanza zitapewa Nambari ya Lalamiko na Secrétaire wa Conférence Générale au Secrétaire wa Malalamiko na kisha zitachapishwa kwenye Toleo la Mapema la *Daily Christian Advocate* na kusambazwa kwa wawakilishi wote na kwa wawakili{ut}shi wa kwanza wachungaji na washirika wa hifadhi angalau siku tisini kabla ya kufunguliwa kwa Conférence Générale. Ripoti zitachapishwa kwa mtindo sawia na *Daily Christian Advocate*. Ili kutimiza haya, nakala kamilifu za ripoti na mapendekezo hayo yote yatawasilishwa kwa mhariri wa *Daily Christian Advocate* angalau siku 230 kabla ya kufunguliwa kwa Conférence Générale.[3] Ripoti na mapendekezo ambayo hayajachapishwa katika Toleo la Mapema la *Daily Christian Advocate* yanaweza kupokewa na Conférence Générale pekee baada ya kura robo tatu za Conférence Générale. Baraza Kuu la fedha na Utawala halitajumuishwa katika hitajiko hili kwa uenezi unaohitajika ili kuruhusu kujumuishwa kwa taarifa ya risiti za fedha jumla za miaka mitatu ya kwanza ya kipindi cha miaka minne. Baraza Kuu la Fedha na Utawala litatoa data ikijumuisha mwaka wa tatu wa kipindi cha miaka minne na taarifa nyingine mwafaka kwa wawakilishi kabla ya kukutana kwa Conférence Générale.

[3] Maoni ya mhariri: *Kitabu kya Adabu kya 2016* ¶ 507.6-7 ilibadilisha tarehe ya mwisho kutoka siku 210 kabla ya kikao cha kufungula cha Conférence Générale hadi siku 230 mbele. Mpango ya Mupangilio na Sheria za Amri zimekuwa update ili kuonyesha mabadiliko yake ya nidhamu.

## SHERIA ZA UTARATIBU

### I. Ratiba ya Kila Siku

*Sheria ya 1. Saa za Mikutano*

Ufuatao utakuwa utaratibu wa kila siku wa Conférence Générale, bila kujumuisha siku ya Jumapili:

(1) 8h00 mupaka maombi na suala ya asubui

(2) 8h20 mupaka 12h30 mukutano wa kikiristo kupitiya planery ama

(3) 13h30 au 14h30 (kama ilivyoonyeshwa na ratiba ya kila siku) mupaka 17h00 kufanya conférence ya kikristo hadi mukutano ya plenary na comité

(4) Wakati wa Huduma ya Ukumbusho, majina ya maaskofu, wake au waume wa maaskofu, na wawakilishi wateule waliofariki tangu kuahirishwa kwa Conférence Générale lililopita yasomwa.

(5) Kipindi cha mapumziko kinaweza kuitishwa wakati wa kikao chochote cha mjadala kwa wakati unaoamuliwa kuwa mwafaka na afisa msimamizi.

(6) Uahirishwaji wa kila siku utaitishwa kufikia saa 18h30 kila jioni, isipokuwa siku ile ambayo mafunzo ya viongozi yameratibiwa na siku ya Jumamosi ambapo uahirishwaji utaitishwa kufikia saa 21h30 usiku. Uahirishwaji utakuwa kawaida kila siku.

*Sheria ya 2. Utaratibu ya Kukongamana kwa Wakristo*

Vikao vya kila siku vya Conférence vitaendeshwa kama ifuatavyo:

(1) Ripoti za comité za utawala na maalum

(2) Ajenda na vipengee vya kalenda

(3) Kalenda ya ridhaa (Tazama Sheria ya 33.5)

(4) Biashara nyingine

### II. Maafisa Wasimamizi

*Sheria ya 3. Mamlaka ya Afisa Msimamizi*

(1) Afisa msimamizi (kikao cha mjadala, comité za utawala, comité za sheria, na comité ndogo) ataamua na kusimamia hoja za utaratibu. Mwakilishi anaweza kukata rufaa kwa uamuzi wa chama bila ya mjadala, hata hivyo afisa msimamizi

na mkata rufaa, kwenye utaratibu uliotajwa hapa, kila mmoja wao atakuwa na dakika tatu za kutoa kauli ya kuunga mkono msimamo wao. Kura sawia katika kesi ya kukata rufaa itamdumisha afisa msimamizi (Tazama Sheria ya 31.5). Mwakilishi yeyote anayeibua hoja ya utaratibu atataja sheria inayoaminika kukiukwa.

(2) Kwa hiari ya afisa msimamizi, muda wa utambuzi wa maombi unaweza kuchukuliwa wakati wa kutafakari. Muda huo unafaa kuwa wa utafakari na maombi ya kundi na utakamilika pindi afisa msimamizi atakaposema hivyo, wakati ambapo kutafakari utaendelea.

(3) Afisa msimamizi atakuwa na haki ya kuitisha kipindi cha mapumziko kwa kikao cha shirika wakati wowote kwa hiari ya afisa msimamizi wakati huo kama vile afisa msimamizi atakavyopendekeza. Kulingana na hali ya roho ya ¶ 722 ya *Kitabu kya Adabu*, katika nyakati nadra afisa msimamizi pia atakuwa na haki ya kukariri kwamba kikao kitakusanyika tena katika kikao kilichofungiwa kilicho na wawakilishi pekee, wafanyikazi walioidhinishwa, na wageni walioidhinishwa na kuruhusiwa kuhudhuria kikao kama hicho kufuatia kuingia kwenye kipindi cha mapumziko (Tazama Sehemu ya VII.G.1.).

*Sheria ya 4. Kuitisha Utaratibu kwenye Conférence*

Wakati afisa msimamizi atakapoitisha utaratibu kwenye shirika, hakuna mwakilishi ataongea, kumhutubia mwenyekiti, wala kusimama.

## III. Haki na Majukumu ya Wawakilishi

*Sheria ya 5. Mahudhurio na Uhifadhi Viti*

(1) Mwenyekiti wa kila uwakilishi atapewa fomu kwa ambayo ataripoti mahudhurio ya kila siku ya wawakilishi wake. Wawakilishi wote wanaowasili baada ya orodha ya usajili ya kufungua kusomwa wataripotiwa na mwenyekiti wa uwakilishi kwa Secrétaire wa Conférence Générale au mteule. Hakuna mwakilishi ambaye amesajiliwa kikamilifu, isipokuwa akizuiliwa na ugonjwa au dharura nyingine, atakosa kuhudhuria vikao vya Conférence bila ruhusa ya Conférence. Wote watakaokosa kuhudhuria wataripotiwa na wenyekiti wa uwakilishi kwa Secrétaire wa Conférence Générale au mteule kwenye fomu inayotolewa kwa dhumuni hili.

(2) Mwakilishi yeyote wa hifadhi aliyejeti mahala pa mwakilishi wa kawaida atakuwa amechaguliwa kikamilifu kama mwakilishi wa hifadhi na Conférence ya Kimwaka na kitatimiza mahitajiko yaliyoelezwa katika *Kitabu kya Adabu* ¶¶ 34-36. Wawakilishi, ikijumuisha wawakilishi wa hifadhi wanapoletwa mahala pa mwakilishi au wawakilishi, watakuwa wameketi kwenye utaratibu wa uchaguzi wao, isipokuwa pale ambapo mwakilishi wa hifadhi ameketi kwa muda tu au katika hitaji maalum kama ilivyoamuliwa na mwenyekiti wa uwakilishi. Mwakilishi wa hifadhi ataketi kwenye kiti cha mwakilishi kwa ambaye badilisho hili linafanywa. Wawakilishi wa hifadhi hawatakuwa wameketi mahala pa wawakilishi wanaowasilisha kwenye jukwaa. Wawakilishi wa hifadhi wanafaa kufanya kazi ndani ya Sheria za Utaratibu wa Conférence Générale (Tazama Sheria 29 na 33). Mwakilishi wa hifadhi anaweza kuketi baada ya mamlaka ya mwenyekiti wa uwakilishi ambaye ataripoti badilisho hilo kwa maandishi kwa Secrétaire wa Conférence Générale au mteule kwenye fomu iliyotolewa kwa dhumuni hili. Wawakilishi wa hifadhi wanachaguliwa ili wameketi:

(1) kwa sababu ya kuwa kwenye utaratibu sawia na wa mwakilishi ambaye hajahudhuria,

(2) katika utaratibu wa kuchaguliwa kwao kama wawakilishi wa hifadhi.

Badilisho hilo likipingwa, Comité ya Stakabadhi baada ya ushauriano na mwenyekiti wa uwakilishi inaweza kuripoti pendekezo lake kwa Conférence Générale.

*Sheria ya 6. Maelekezo ya Kuhifadhi Jumba la Mjadala*

Mwakilishi anayetamani kuhutubia Conférence ili kusajili kwa namna ulivyobainishwa. Askofu msimamizi atachagua kutoka kwa maombi, kudakiza taratibu, na kumwelekeza msemaji kwa kipaza sauti mwafaka. Askofu msimamizi atazingatia sehemu mbalimbali za jumba la mjadala kwa mzunguko. Mwakilishi anayetambuliwa ataelekea kwenye kipaza sauti kilicho karibu zaidi naye na kwanza atatangaza jina lake na jina la conférence anayowakilisha na sababu yake ya kuongea. Mwakilishi aliyetambuliwa na askofu msimamizi hawezi kupatiana nafasi yake kwa mwakilishi mwingine. Endapo tarakilisi kibao kikose kufanya kazi, mwakilishi anayetamani kuhutubia Conférence atainua juu kibao mwafaka ili kitambuliwe na askofu msimamizi.

*Sheria ya 7. Wasemaji wa Mjadala Wanaounga Mkono na Wanaopinga*

(1) Wakati ripoti ya comité inapozingatiwa, litakuwa jukumu la askofu msimamizi kuthibitisha, wakati anamtambua mwakilishi kwenye Conférence, ni upande gani huyo mwakilishi anataka kuunga mkono, askofu msimamizi hatapeana nafasi ya kuongea kwa mwakilishi yeyote anayependekeza kuongea kwa kuunga mkono upande sawia na ule wa msemaji aliyemtangulia wakati huo huo ikiwa mwakilishi angependa kuongea akiunga mkono upande ule mwingine.

(2) Isipokuwa maazimio yasiyoweza kujadiliwa (Sheria ya 23), hakuna ripoti itakubalika na kutumika au swali linalohusiana na azimio hilo litaamuliwa, bila ya fursa kupewa angalau batu bawili banounga mkono na bawili banaopinga pendekezo hilo.

(3) Azimio la kuitisha swali la awali ambalo kivyake haliwezi kujadiliwa, halitakuwa kwenye utaratibu bila ya fursa kupewa angalau batu bawili banaounga mkono na bawili banaopinga pendekezo hilo. Mwakilishi yeyote anayeibua swali la awali (yaani, kwamba kura ipigwe kuhusu azimio hilo au maazimio yaliyosubirishwa) pia ataonyesha ni nini pia kinakusudiwa kutumika, ikiwa maazimio yoyote yasiyo msingi au maazimio pia yanasubirishwa. Mwakilishi huyo asipoonyesha hivyo, itachukuliwa kwamba anatuma ombi tu la swali ambalo limesubirishwa. Azimio hili litachukuliwa bila mjadala na litahitaji kura thuluthi mbili za wale waliopo na wanaopigia kura kukubaliwa na kutumiwa kwake. Ikikubaliwa na kutumiwa, kura itapigiwa azimio au maazimio kwa ambayo inatumika bila mjadala wa ziada (Tazama Sheria ya 23). Baada ya hotuba tatu za kuunga mkono na tatu za kupinga na mradi tu hakuna maazimio yasiyo msingi yaliletwa mbele ya kikao, basi maswali yataulizwa kiotomati. Hata hivyo, mwenyekiti na/au mwakilishi aliyeidhinishwa kikamilifu au wawakilishi wanaowasilisha ripoti ya comité, na ikiwa kuna ripoti ya wachache, mwasilishaji atakuwa na haki ya kuzungumza kabla ya kura kupigwa (Tazama Sheria ya 29). Hotuba hizi zitapewa tu muda wa dakika tatu (3) (Tazama Sheria ya 9). Baada ya discours tatu zinazounga mukuno na tatu za kupinga, ikiwa kuna mada ingine kwenye sakafu, mada ya kurudia swali la hapo awali haiwezi kujadiliwa na itapigiwa kura baada ya msimamiaji kutoa idadi ya wasemaji wanaounga mukono na wanaopinga, na marekjebisho.

*Sheria ya 8. Kumdakiza Msemaji*

Hakuna mwakilishi aliye kwenye jukwaa anaweza kudakizwa isipokuwa kwa ajili ya hoja ya utaratibu, uchunguzi wa bunge, hoja ya taarifa, au kuitisha umakinifu kwamba muda umetimia wa utaratibu wa siku.

*Sheria ya 9. Kuzungumza Zaidi ya Mara Moja; Urefu wa Hotuba*

(1) Hakuna mwakilishi atazungumza mara ya pili kuhusu swali sawia ikiwa mwakilishi yeyote ambaye hajazungumza hapo awali kuhusu swali hilo anataka kuchangia kwenye jukwaa.

(2) Hakuna mwakilishi atazungumza zaidi ya mara mbili kuhusu mada sawia chini ya azimio sawia, isipokuwa kama ilivyoelezewa katika Sheria ya 7.2

(3) Hakuna mwakilishi atazungumza zaidi ya dakika tatu isipokuwa muda wake uwe umeongezwa na shirika (Tazama Sheria ya 7.3). Muda wa utafsiri hautahesabiwa kwenye kipimo cha dakika tatu kilichowekwa.

(4) Kipimo cha dakika tatu kilichowekewa hotuba za wawakilishi kinaweza kurekebishwa kwa kura ya wengi kwenye shirika wakati wowote na kwa kipindi chochote cha muda.

*Sheria ya 10. Hoja ya Utaratibu*

Mwakilishi anayetaka kuibua hoja ya utaratibu andikisha ombi kwa njia iliyoelezewa na Tume ya Conférence Générale na kufafanuliwa na msimamizi. Afisa msimamizi atadakiza taratibu. Ikiwa mwakilishi anazungumza, huyo atachukua jukwaa mara moja na kutoa hoja yake. Afisa msimamizi kisha atamwelekeza mwakilishi anayeibua hoja ya utaratibukwanza ataje sheria husika na kisha kueleza hoja kwa ufupi na kwa uhakiki iwezekanavyo. Mwakilishi hataishia kuamua swali husika wala kujadili hoja hiyo. Hoja ya utaratibu inaamuliwa na afisa msimamizi bila mjadala isipokuwa tu katika matukio yanayotia shaka afisa msimamizi anawasilisha swali hilo kwa shirika ili kupata ushauri au uamuzi. Wakati afisa msimamizi anapoamua kuhusu hoja, mjadala unafungwa, lakini uamuzi huo unaweza kukatiwa rufaa (Tazama Sheria ya 3).

*Sheria ya 11. Waamuzi wa Conférence*

Waamuzi wa conférence watatoa uadilifu wa Conférence Générale. Ni kwa wawakilishi, kurasa na wengine ambao wamepewa ufikiaji kwa eneo la

shughuli ya Conférence Générale kama ilivyoelezewa kupitia Sheria au kupitia kwenye uahirishaji Sheria.

*Sheria ya 12. Tabia Inayokengeusha*

Roho ya kukongamana kwa Wakristo inatarajiwa. Bajumbe habafae kusumbua bengine. Matumizi ya simu ya mkononi inayosikika hayaruhusiwi katika jumba la mjadala au vyumba vya comité ya sheria. Vifaa vyote vya kielektroniki vitawekwa kimya au kuzimwa. Kwa ziada, matumizi ya vifaa vya kielektroniki yanafaa kuwa kwa namna ambayo haiwasumbui washiriki wengine. Heshima itaonyeshwai katika matumizi ya mitandao wa kijamii nyakati zote. Ukengeushaji kwa matamshi na usio kwa matamshi haviruhusiwi. Afisa msimamizi au wafanyikazi wa Conférence Générale wanaweza kuomba watu binafsi kuondoka kwenye jumba la majadala au chumba cha comité ya sheria wakiendelea na tabia inayohitilafiana na ushiriki kwa wawakilishi wengine.

*Sheria ya 13. Kurekodi Kielektroniki*

Hakuna kurekodi kielektroniki kwa aidha video au sauti kunaweza kufanyiwa sehemu yoyote ya Conférence Générale isipokuwa kama kumeidhishwa kimahsusi na Meneja wa Biashara wa Conférence Générale ili kudumisha uadilifu wa leseni zote za utendakazi.

*Sheria ya 14. Haki ya Kutoa Maazimio*

Ni wawakilishi tu wanaopiga kura walio na haki ya kutoa au kuunga mkono maazimio kulingana na sheria na baada ya kutambuliwa na afisa msimamizi.

*Sheria ya 15. Utaratibu wa Kupiga Kura kwenye Jumba la Mjadala*

(1) Upigaji kura utafanywa kwa njia za kielektroniki isipokuwa kama imeamrishwa vinginevyo na Conférence, hata hivyo, mradi tu katika uchaguzi, upigaji kura unaweza kuwa kwa kura za karatasi. Vifaa vya kupigia kura vya kielektroniki vitapatikana kwenye jukwaa kwa minajili ya wawakilishi wanaowasilisha kwa Conférence.

(2) Wakati upigaji kura kielektroniki hautumiki au haufanyi kazi, hesabu ya kura kwa kusimama au kwa kura ya za karatasi inaweza kuitishwa na mwakilishi yeyote, akiungwa mkono na thuluthi moja ya wawakilishi waliopo na upigaji kura kufanywa kwa kutumia kurasa zinazohudumu kama basimamiaji upigaji kura.

(3) Ni wawakilishi tu walio ndani ya waamuzi wa conférence wakati kura inapopigwa watakaokuwa na haki ya kupiga kura. Hakuna mwakilishi atapiga kura kwa niaba ya mwakilishi yeyote mwingine.

(4) Hakuna biashara nyingine itakayoendelea wakati kura inapopigwa au wakati swali la awali limetajwa mpaka pale mchakato huu utakapokamilika, isipokuwa tu kama inahusu kura yenyewe au shughuli hiyo kama vile afisa msimamizi anavyoweza kuona inafaa.

(5) Bajumbe biko huru kupiga kura kulingana na dhamiri zabo bila kuingiliwa na bengine kutazama, kuangalia, ao kurekodi kura zabo. Batu habatatoa ao kupokea bongo ao kutishia bajumbe juu ya kushawishi kupiga kura.

*Sheria ya 16. Uchaguzi*

Kwa uchaguzi wowote unaohitaji kikao cha mjadala kupiga kura, uchaguzi utafanyika wakati idadi ya kura zilizopigiwa mteule zinafikia au kuzidi ile asilimia inayohitajika ya kura halali jumla.

Kura ni halali ikiwa imetimiza viwango vifuatavyo:

(1) Imepigwa na mwakilishi anayestahili kupiga kura au mwakilishi wa hifadhi mwenye kiti mwafaka.
(2) Ina kura za idadi sawia ya wateule, kama idadi ya nafasi zinazotakiwa kujazwa.
(3) Kila jina linalopokea kura limeteuliwa vifaavyo kulingana na misimamo iliopo.
(4) Hakuna kura zaidi ya moja inapigiwi mteule sawia.
(5) Hakuna kura inapigiwa mtu ambaye tayari amechaguliwa.

*Sheria ya 17. Kitengo cha Swali*

Kabla ya kura kupigwa, mwakilishi yeyote atakuwa na haki ya kuitisha kitengo cha swali lolote, ikiwa swali hilo linahusu kitengo hicho kama vile mwakilishi anavyoashiria. Ikiwa hauna mwakilishi anayepinga, kitengo hicho kitatolewa; lakini ikiwa kuna pingamizi, afisa msimamizi ataweka swali la kitengo kupigiwe kura, bila kusubiri kuungwa mkono.

## IV. Tabia za Wageni na Waangalizi

*Sheria ya 18. Tabia Inayokengeusha*

Roho ya kukongamana kwa Wakristo inatarajiwa. Wageni na Waangalizi hawafai kuwakengeusha wengine. Matumizi ya simu ya mkononi inayosikika hayaruhusiwi katika jumba la mjadala au vyumba vya comité ya sheria. Vifaa vyote vya kielektroniki vitawekwa kimya au kuzimwa. Kwa ziada, matumizi ya vifaa vya kielektroniki yanafaa kuwa kwa namna ambayo haiwasumbui washiriki wengine. Heshima itaonyeshwai katika matumizi ya mitandao wa kijamii nyakati zote. Ukengeushaji kwa matamshi na usio kwa matamshi haviruhusiwi. Afisa msimamizi au wafanyikazi wa Conférence Générale wanaweza kuomba watu binafsi kuondoka kwenye jumba la majadala au chumba cha comité ya sheria wakiendelea na tabia inayohitilafiana na ushiriki kwa wawakilishi. Wageni na waangalizi hawafai kuingia eneo la waamuzi wa conférence isipokuwa tu kama ilivyoelezewa katika Sheria ya 11.

*Sheria ya 19. Kurekodi Kielektroniki*

Hakuna kurekodi kielektroniki kwa aidha video au sauti kunaweza kufanyiwa sehemu yoyote ya Conférence Générale isipokuwa kama kumeidhishwa kimahsusi na Meneja wa Biashara wa Conférence Générale ili kudumisha uadilifu wa leseni zote za utendakazi.

## V. Utaratibu wa Biashara

*Sheria ya 20. Azimio la Kukubaliwa na Kutumiwa kwa Ripoti za Comité za Sheria na Utawala*

Wakati wowote ripoti ya comité ya sheria au comité ya utawala inapowasilishwa kwa Conférence ili hatua ichukuliwa, itachukuliwa kuwa utaratibu unaofaa ili kuzingatiwa na Conférence bila ya urasmi wa kuungwa mkono.

*Sheria ya 21. Fomu Zinazohitajika kwa Ripoti, Suluhu, Maazimio, Marekebisho*

Suluhu zote na ripoti za comité zitatayarishwa kulingana na maelekezo kutoka kwa Secrétaire wa Conférence Générale; na maazimio yote, ikijumuisha marekebisho, yatawasilishwa kwa maandishi (Tazama Sheria za 33.2, 34.3, 36.2, 38).

*Sheria ya 22. Mabadiliko ya Maazimio*

Wakati azimio linapotolewa na kuungwa mkono, suluhu inaletwa na kuungwa mkono, au ripoti ya comité inasomwa au kuchapishwa kwenye *Daily Christian Advocate*, itaonekana kuwa katika umiliki wa Conférence na haiwezi kubadilishwa isipokuwa kwa hatua ya Conférence (Tazama Sheria ya 39).

*Sheria ya 23. Maazimio Yasiyoweza Kujadiliwa*

Maazimio yafuatayo yatashughulikiwa bila mjadala:

(1) Kuahirisha, wakati haujafuzu, isipokuwa tu kwa uahirishwaji wa mwisho.

(2) Kusitisha sheria.

(3) Kuweka mezani.

Hakuna azimio, ambalo linaambatana azimio lingine au lina azimio lingine linaloambatana nalo, linaweza kuwekwa mezani lenyewe. Maazimio kama hayo, yakiwekwa mezani, yanaandamana na maazimiokwa ambayo yanaambatana au yale yanayoambatana nayo.

(4) Kuchukua mezani.

(5) Kuyaita maswali ya awali, ikiwa katika utaratibu (Tazama Sheria za 7 na 24).

(6) Kuzingatia tena azimio lisiloweza kujadiliwa (Tazama Sheria ya 32)

(7) Kuwekea mipaka au kupanua mipaka ya mjadala.

(8) Kuchukua muda kwa ajili ya utambuzi wa kimaombi wakati ufaao.

(9) Kuomba uamuzi wa Conseil ya Mahakama (*Kitabu kya Adabu* ¶¶ 56.1, 2609.1).

*Sheria ya 24. Haki za Swali Kuu*

Swali kuu linaweza kujadiliwa chini ya maazimio yafuatayo: kukubaliwa na kutumika, kutumwa, kubadilisha, kuahirishwa au kuzingatiwa tena. Hakuna azimio, suluhu, au mada mpya zitaruhusiwa mpaka pale ambapo lile linalozingatiwa litakapomaliziwa isipokuwa tu kama ilivyoelezwa katika Sheria ya 15.4. Sheria hii haitumiki kwa maazimio yasio msingi ikiwa vinginevyo inaruhusiwa.

*Sheria ya 25. Kipaumbele cha Maazimio yasiyo Msingi*

Kama mmoja au zaidi ya maazimio yafuatayo yatafanywa wakati azimio lingine moja au zaidi yangali yanasubirishwa, utaratibu wa kipaumbele cha maazimio hayo ikilinganishwa na mengine utakuwa sawia na utaratibu wa kuorodheshwa kwake hapo chini:

(1) Kurekebisha muda ambao conférence itaahirishwa (Azimio hili linaweza kurekebishwa, au linaweza kuwekwa mezani.);
(2) Kuahirisha;
(3) Kufanya mapumziko;
(4) Kuweka mezani;
(5) Swali yenye ilipita (Tazama Sheria ya 23.5, 28);
(6) Kuwekea mipaka au kupanua mipaka ya mjadala;
(7) Kuahirisha hadi muda fulani;
(8) Kutumwa;
(9) Kurekebisha au kurekebisha kwa kubadilisha (rekebisho moja likiruhusiwa badala ya rekebisho lingine);
(10) Kuahirisha hadi wakati usiojulikana.

*Sheria ya 26. Azimio la Kuahirisha*

Azimio la kuahirisha, wakati halijafuzu, litachukuliwa bila mjadala na kila wakati litakuwa katika utaratibu, isipokuwa:

(1) Wakati mujumbe ana jukwaa;
(2) Wakati swali linapoulizwa au kura inapigwa na kabla mwisho kuamuliwa;
(3) Wakati swali yenye ilipita na hatua inangojewa;
(4) Wakati wa azimio la kuahirisha halijafaulu na hakuna biashara au mjadala umeingilia katikati;
(5) Wakati azimio la kurekebisha muda kwa ambao Conférence litaahirishwa linangojewa.

Sheria hii haitumiki kwa azimio la uahirishwaji wa mwisho wa Conférence.

*Sheria ya 27. Uahirishwaji wa Mwisho*

Katika uahirishwaji wa mwisho biashara zote ambazo hazijakamilika zitasalia vivyo hivyo.

*Sheria ya 28. Utaratibu wa Kurekebisha kwa Kubadilisha*

(1) Wakati suluhu au ripoti ya comité imeletwa vifaavyo mbele ya Conférence ili kuzingatiwa na hatua kuchukuliwa, hata kama marekebisho yanasubiriwa, badilisho linaweza kutolewa na mwakilishi yeyote akipendekeza kwamba marekebisho hayo yabadilishiwe mahala pa ripoti, suluhu au rekebisho linalozingatiwa. Badilisho hilo litakuwa mbadala ya kile kilicho mbele ya shirika na wala sio tu ukanushaji wa azimio kuu.

(2) Mjadala wa azimio la kubadilisha utakuwa tu wa swali la kubadilisha pekee. Hakuna marekebisho kwa azimio kuwa au badilisho yatazingatiwa wakati wa kipindi hiki cha uzingatiaji wa kwanza.

(3) Kufuatia mjadala wa azimio la kubadilisha, kura ya kubadilisha itapigwa. Azimio la kubadilisha likishinda kwa kura ya wengi, basi azimio la kubadilisha linakuwa azimio kuu. Azimio la kubadilisha likishindwa kutopokea kuraya wengi, azimio kuu asilia linasalia kujadiliwa ili kuzingatiwa. Mjadala unaojumuisha kutolewa kwa marekebisho unasonga mbele kwenye azimio kuu kulingana na sheria za utaratibu.

(4) Azimio la kuita maswali ya awali halitakuwa katika utaratibu kwenye azimio la kubadilisha mpaka pale ambapo fursa imetolewa kwa angalau wasemaji wawili wa kila upande kuhusu swali hilo.

*Sheria ya 29. Ripoti ya Wachache*

Ripoti ya wachache inaweza kuambatishwa katika ripoti kutoka kwa comité ya sheria kwa namna ifuatayo:

> (1) Wawakilishi wanaonuia kutoa ripoti ya wachache ni lazima wamfahamishe mwenyekiti wa comité ndani ya saa mbili (bila kuhesabu mapumziko) za hatua ya mwisho ya comité kuhusu lalamiko husika.
>
> (2) Mwenyekiti wa comité ya sheria atapokea ripoti ya wachache iliyotiwa sahihi na watu 10 au 10% ya ushirika wa comité ya sheria (yoyote ile iliyo chache) waliopiga kura wakipinga pendekezo hilo, ambao majina yao yataambatishwa kwenye ombi hilo. Mwakilishi wa hifadhi anaweza kutia sahihi ripoti ya wachache akiwa tu akiwa ameketi

kama mujumbe katika comitté ua sheria_wakati comité iliposhughulikia lalamiko husika. Comité na ripoti za wachache vitatumwa na kuwasilishwa pamoja katika *Daily Christian Advocate*.

(3) Ripoti ya wachache itawasilishwa kama badilisho kwa ripoti ya comité, kwa kuambatana na Sheria ya 28 na Sheria ya 36 mtawalia, na itasimamiwa katika jumba la mjadala kulingana na Sheria ya 28 kwa maazimio ya badilisho. Waliotiaa sahihi kwenye ripoti ya wachache watamteua mmoja wao kuwasilisha ripoti kama azimio la badilisho. Katika mjadala wa kufunga kuhusiana na azimio la badiliso, mwakilishi anayewasilisha ripoti ya wachache atazungumza kwanza naye mwasilishaji wa ripoti ya comité atakuwa wa mwisho.

(4) Azimio la kubadilishia ripoti ya wachache kwa ripoti ya wengi likifuzu kwa kura ya wengi katika kikao cha mjadala, basi ripoti ya wachache inakuwa ndiyo azimio kuu. Azimio la kubadilisha likishindwa kufuzu kwa kura ya wengi katika kikao cha mjadala, ripoti ya wengi ya comité inasalia kujadiliwa kama azimio kuu la kuzingatiwa. Mjadala unaojumuisha kutolewa kwa marekebisho unasonga mbele kwenye azimio kuu kulingana na sheria za utaratibu.

*Sheria ya 30. Azimio Lisilofuata Sheria Baada ya Hotuba*

Baada ya kutoa hotuba kuhusu swali lililosubirishwa, mwakilishi hawezi kutoa azimio ambalo litawekewa mipaka au kusitisha mjadala bila kwanza kuondoka jukwaani.

*Sheria ya 31. Ubaguzi kwa Kura ya Wengi{*

Wengi wa wanaopiga kura, akidi ikiwepo (*Kitabu kya Adabu* ¶ 506), wataamua maswali yote, huku kukiwa na ubaguzi ufuatao:

(1) Kura humsi moja za Conférence zitahitajika ili kuagizia uamuzi wa Conseil ya Mahakama (*Kitabu kya Adabu* ¶¶ 56.1, 2609.1).

(2) Kura humsi moja za Conférence zitatuma suala kwa ya Comité ya Maadili.

(3) Mtu ambaye sio mwakilishi anaweza kualikwa kwenye comité kamili au comité ndogo ya sheria aidha kupitia mwaliko wa mwenyekiti au kwa kura thuluthi moja (1/3) za shirika lolote ili kuzungumzia suala lolote moja kwa muda usiozidi dakika tatu (3).

(4) Thuluthi moja ya waliopo kuwepo na wanaopiga kura itatosha kuruhusu mwito wa upigaji kura ulirekodiwa endapo uamuzi wa afisa msimamizi utapingwa (Tazama Sheria ya 15.2).

(5) Matokeo ya kura kutoshana yanaunga mkono afisa msimamizi (Sheria ya 3.1).

(6) Kura thuluthi mbili zitahitajika ili kuendeleza azimio la kusitisha (Sheria ya 40) au kurekebisha (Sheria ya 41) sheria; ili kuweka kando utaratibu maalum (Sheria ya 33.1); ili kuzingatia utaratibu maalum kabla ya wakati uliopangwa; ili kukubali ombi la Comité ya Hisani na Fadhila kwa wasilisho la mtu yeyote baada ya siku ya sita ya Conférence Générale (Tazama Sehemu ya VII.A.3).

(7) Kura thuluthi mbili zitahitajika ili kuendeleza kuitwa kwa swali la awali.

(8) Kura thuluthi mbili zitahitajika ili kuidhinisha pendekezo la marekebisho ya katiba (*Kitabu kya Adabu* ¶¶ 59-61).

*Sheria ya 32. Uzingatiaji Tena*

Azimio la kuzingatia tena hatua ya shirika litakuwa katika utaratibu wakati wowote kama litatolewa na mwakilishi aliyepiga kura wa upande ulioshinda. Ikiwa azimio lililopendekezwa kuzingatiwa tena lilikuwa lisiloweza kujadiliwa, azimio la kuzingatiwa tena litakuwa lisiloweza kujadiliwa (Tazama Sheria ya 23).

*Sheria ya 33. Kalenda ya Kawaida na Kalenda ya Ridhaa*

(1) Secrétaire wa Conférence Générale atahifadhi Kalenda inayojumuisha taratibu za siku na ripoti za comité (Tazama Sheria ya 39). Biashara iliyowekwa kwenye kalenda itazingatiwa katika utaratibu uliopendekezwa na Comité ya Ajenda na Kalenda, isipokuwa kwa kura thuluthi mbili za Conférence, kipengee kinashughulikiwa nje ya utaratibu. (Tazama Sheria ya 31.6).

(2) Wakati wowote inapowezekana, comité ya sheria itapendekeza kukubaliwa na kutumika kwa kipengee kimoja tu cha kalenda kwa kila aya au aya ndogo katika *Kitabu kya Adabu*. Malalamiko mengine yote husika yataunganishwa ili kukataliwa au kutumwa.

(3) Hatua kutoka kwa comité ya sheria itawekwa kwenye Kalenda ya Ridhaa ikiwa:

(a) Kura zisizozidi kumi zilipigwa dhidi ya upande ulioshinda katika comité;
(b) Kipengee hicho kimechapishwa hapo awali katika *Daily Christian Advocate*;
(c) Kipengee hicho kimekuwa mikononi mwa wawakilishi kwa angalau saa 24;
(d) Kipengee hicho sio rekebisho la katiba wala chneye athari za kifedha; na
(e) Hakuna ripoti ya wachache imeambatishwa (Tazama Sheria ya 29).

(4) *Daily Christian Advocate* itatambulisha waziwazi Kalenda ya Ridhaa, ambayo itaorodhesha vipengee kwa sehemu tatu zenye vichwa vidogo kama ifuatavyo:

(a) Vipengee vya Kinidhamu, Vilivyopendekezwa Kukubaliwa na Kutumika.
(b) Vipengee Visivyo vya Kinidhamu Vilivyopendekezwa Kukubaliwa na Kutumika.
(c) Vipenge Vilivyopendekezwa Kupigwa Rufaa.

(5) Kalenda ya Ridhaa itaitwa kila siku kuambatana na Sheria ya 2. Kukubaliwa na kutumiwa kwa Kalenda ya Ridhaa kwa kura ya Conférence kutaonekana kuwa hatua kwenye vipengee vyote vya Kalenda kwenye Kalenda ya Ridhaa.

(6) Kasoro katika kupeana kipengee cha Kalenda ya Ridhaa ikigunduliwa na kuripotiwa na mwenyekiti wa sheria kwa Mratibu wa Kalenda, Mratibu wa Kalenda atakuwa na mamlaka ya kuripoti kasoro hiyo kwa kikao cha mjadala ili kuzingatiwa tena.

(7) Wawakilishi wowote 20 wanaweza kukiondoa kipengee cha Kalenda ya Ridhaa kwa kuandikisha ombi lao kwa Secrétaire wa Conférence Générale kufikia 15h00 za siku ambayo kipengee hicho cha kalenda kinaonekana kwa mara ya kwanza katika *Daily Christian Advocate*. Bawakilishi wa hifadhi wanaweza kutia sahihi maombi ya kuondoa

vipengee kutoka kwa Kalenda ya Ridhaa wakiwa tu wameketi kama wawakalishi wapiga kura. Vipengee hivyo vitaitwa kwa utaratibu wa kawaida wa biashara.

(8) Vipengee vilivyoondolewa kwenye Kalenda ya Ridhaa haviwezi kurudishwa kwenye Kalenda ya Ridhaa.

*Sheria ya 34. Ripoti ya Vipengee Visivyo kuwa vya Kalenda*

(1) Kwa kuongezea kwa vipengee vya kalenda vya kuwakilishwa kwa kikao cha mjadala, kila comité ya sheria itaripoti vipengee vyote ambavyo havijawasilishwa kwa kategoria zifuatazo:[4]

a) Maombi hayatafanywa kwa sababu ya pendekezo jingine kwenye somo moya.

b) Malalamiko ambayo hayajaungwa mkono na comité ya sheria. Comité itaripoti kura ya comité.

(2) Ripoti hizi katika *Daily Christian Advocate*.

(3) Wawakilishi wowote 20 wanaweza kufanya kipengee katika (1)(b) kilichotajwa hapo juu kuwasilishwa kwa kikao cha mjadala kwa kuweza kuandikisha ombi hilo kwa Secrétaire wa Conférence Générale kufikia 15h00 za siku ambayo kipengee hicho kinaonekana kwa mara ya kwanza katika *Daily Christian Advocate*. Wawakilishi wa hifadhi wanaweza kutia sahihi maombi ya kuwasilisha kipengee katika (1)(b) hapo juu ikiwa tu wameketi kama wawakilishi wapiga kura. Vipengee hivyo vitaitwa katika utaratibu wa kawaida wa biashara wakati mwenyekiti wa comité husika yuko jukwaani. Wale wanaounga mkono kuzingatiwa kwa vipengee hivyo watateua mmoja wao kuwasilisha kipengee hicho kwa kikao cha mjadala.

*Sheria ya 35. Sheria za Utaratibu wa Comité za Sheria*

Sheria za utaratibu wa Conférence Générale, isipokuwa Sheria ya 7, zitazingatiwa katika mikutano ya comité za sheria za kudumu mradi tu ziwe zinatumika.

*Sheria ya 36. Majukumu na Haki Maalum za Comité za Sheria*

---

[4] Maoni ya mhariri: *Kitabu kya Adhabu kya 2016* ¶ 507.11 inahitaji kwamba maombi zote zinapashwa kuwasilishwa kwa Mkutano Mkuu itapokea kura ya comité ya kisheria. Sheria ya 34.1 imefanyiwa update na Sheria ya zamani ya 37 imefutwa ili kuonyesha mabadiliko haya ya kinidhamu.

(1) Baada ya maafisa kuelezwa kuhusu kazi zao, uongozi wa comité, ukitumia rasilimali za mratibu wao wa malalamiko, utatathmini malalamiko yaliyopewa comité, kuweka kipaumbele, na kuainisha kazi ya comité kimsingi na kipaumbele isipokuwa tu kama imepewa maelekezo maalum na Conférence Générale (Tazama Sehemu ya VII.A.(7)(a)).

(2) Mwenyekiti wa comité ndogo ya sheria atahakikisha kwamba kura zote ndani ya comité ndogo zimerekodiwa na kuripotiwa kwa kikao cha mjadala cha comité ya sheria kwenye fomu zilizotolewa na Secrétaire wa Conférence Générale.

(3) Wakati lalamiko au suluhu au kipengee chochote sawia kinatumwa kwa comité moja ya comité za sheria, itaeleweka kwamba swali nzima linalohusu kipengee hicho limetumwa kwa comité hiyo ili kuchukuliwa hatua mwafaka. Kila suala linaloungwa mkono na comité ya sheria litaripotiwa kwa kikao cha mjadala kwa azimio la kulikubali na kulitumia aidha lichukuliwe hatua au lijumishwe katika ripoti kwa Conférence Générale lijalo.

(4) Comité zitaripoti kwa Conférence baada ya masuala yote yaliyotumwa kwao na Conférence, moja kwa moja au kupitia Comité ya Marejeleo. Ripoti za comité za suluhu, malalamiko, n.k., zitataja masuala sawia, zikiyatambulisha kwa nambari zilizo nazo katika ripoti zilizochapishwa za Comité ya Marejeleo au kwa namna nyingine inayofaa.

(5) Wakati comité inapothibitisha kwamba comité nyingine inazingatia au kwa uamuzi wake inafaa kuwa ikizingatia, mada, ambayo comité hiyo nyingine inazingatia, itaripoti suala hilo kwa Comité ya Marejeleo ili rekebisho hilo kifanywe kulingana na vile hali inavyohitaji.

(6) Mwenyekiti wa kila comité ya sheria ataratibu ripoti ya comité kwa kikao cha mjadala.

(7) Wakati mwenyekiti wa comité hakubaliani na ripoti iliyokubaliwa na kutumiwa na comité, basi litakuwa jukumu la mwenyekiti kutaja hoja hiyo kwa comité. Comité itamteua mmoja wa wanachama wake kuwasilisha na kujadili ripoti hiyo katika kikao cha mjadala. Ikiwa, katika hali kama hiyo, comité

itashindwa kumteua mwakilishi, mwenyekiti atamteua mwanachama mmoja kuwakilisha comité, naye mwakilishi huyo atakuwa na haki na fadhila zote za mwenyekiti kuhusiana na ripoti kama hiyo.

*Sheria ya 37. Ripoti ya Comité ya Sheria kwa* Daily Christian Advocate

(1) Vile nyenzo zinavyoweza kutayarishwa haraka, kila secrétaire wa comité ya sheria atawasilisha kila moja ya ripoti za comité kwa mtu anayerekodi aliyeteuliwa na comité. Mtu anayerekodi atatayarisha ripoti na ripoti hiyo itaidhinishwa na kutiwa sahihi na mwenyekiti, makamu mwenyekiti na secrétaire. Baada ya ripoti kuidhinishwa, itatumwa kielektroniki kwa Mratibu wa Kalenda. Ripoti hiyo itapewa nambari ya kalenda na kucahpishwa kuwa imeidhinishwa.

(2) Ripoti za comité na za wachache zinazopendekeza mabadiliko katika *Kitabu kya Adabu* zitatoa nambari ya aya inayoathirika na itatayarishwa kwa namna ifuatayo: Maneno yaliyotumiwa kama marejeleo yatakuwa ndani ya alama za usemi; maneno ya kufutwa yatatiwa mstari wa mlazo; na maneno ya kuongezwa yatakuwa kwa wino kolevu. Katika uchapishaji wa ripoti hizi, *Daily Christian Advocate* itatumia mpangilio sawia (Tazama Sheria ya 40).

*Sheria ya 38. Ripoti Zilizochapishwa Zinazomilikiwa na Conférence*

Ripoti zinazowasilishwa na Comité kulingana na wakati wa mwisho, kama ilivyotangazwa na Secrétaire wa Conférence Générale, zitaonekana kwenye *Daily Christian Advocate* ya siku inayofuata. Vile ripoti hiyo imechapishwa katika *Daily Christian Advocate* ndiyo nakala rasmi, inayoweza tu kufanyiwa marekebishio ya kisarufi, au mabadiliko mengine ya kawaida ya uhariri na itachukuliwa kuwa inamilikiwa na Conférence. Kwenye siku itakayofuatia siku ambayo *Daily Christian Advocate* ilipoonekana kwa mara ya kwanza au wakati wowote baadaye, ripoti imo katika utaratibu wa kuzingatiwa kwa mapenzi ya conférence. Sheria sawia itatumika kwa ripoti ya wachache kutoka comité yoyote (Tazama Sheria za 22, 29).

*Sheria ya 39. Utayarisho na Uchapishaji Ripoti*

(1) Ripoti zote za comité zitatayarishwa kwa kutumia Mfumo wa Sheria wa Conférence Générale na Tume ya Conférence Générale.

(2) Ripoti kwa Mratibu wa Kalenda kwa vipengee vilivyopigiwa kura katika comité itajumuisha jina la comité hiyo, jumla ya wanachama, idadi ya waliopo wakati kipengee hicho kilipokubaliwa na kutumiwa, na idadi ya wanaopigia kura kipengee hicho kwa kukiunga mkono na kutokiunga mkono.

(3) Ripoti za comité za sheria zitachapishwa katika *Daily Christian Advocate* angalau siku moja kabla ya kuwasilishwa ili kuzingatiwa na Conférence. Ripoti za comité zenye ripoti za wachache zitachapishwa kwa mpangilio, na kupewa nambari.

(4) Kila juhudi inafaa kufanywa na secrétaire wa comité ya sheria ili kuripoti malalamiko yote mtawalia yanayoangazia suala sawia.

## VI. Kusitisha, Kurekebisha, na Kuongezea

*Sheria ya 40. Kusitishwa Sheria*

Operesheni ya yoyote ya misimamo ya Mpango wa Mupangilio na Sheria za Utaratibu inaweza kusitishwa kwa wakati wowote kwa kura thuluthi mbili za Conférence (Tazama Sheria ya 31.6).

*Sheria ya 41. Kurekebisha Sheria*

Mpango wa Mipangilio na Sheria za Utaratibu unaweza kurekebishwa au kubadilishwa kwa kura thuluthi mbili za Conférence; mradi tu mabadiliko au marekebisho yaliyopendekezwa yametoka kwa Comité ya Mpango wa Mipangilio na Sheria za Utaratibu au yamewasilishwa kwa Conférence kwa maandishi na kutumwa kwa comité hii, ambapo comité itaripoti kabla ya siku inayofuata kuisha (Tazama Sheria ya 31.6).

Mpango wa Mipangilio na Sheria za Utaratibu kama ulivyokubalika na kutumika kwenye kikao cha kufungua utachapishwa katika *Daily Christian Advocate*.

*Sheria ya 42.* Sheria za utaratibu za Robert*, Mamlaka Saidizi*

Katika hali yoyote ya bunge ambayo haijajumuishwa katika Mpango wa Mipangilio na Sheria za Utaratibu, Conférence Générale litaongozwa katika hatua yake na toleo la sasa la *Sheria za Utaratibu za Robert*.

## Regles ya 33. Calendrier yenye Inapeana Ruhusa

Mambo za kutazamiya ku calendrier zinawekewaka kiotomatiki mu calendrier yenye inapeana ruhusa wakati kipengele kina kura kumi (10) ao kidogo contre nafasi yenye iko ya kamati ya sheriya. Regles ya 33(3)(a)

Kuna ma calendrier tatu tafauti zenye zinapeana ruhusa:

- Calendrier yenye Inapeana Ruhusa A ina mambo za kutazamiya ku calendrier zenye zinahusisha mabadiliko ya adabu ambayo pendekezo ya kamati ya sheriya inapashwa kupitisha
- Calendrier yenye Inapeana Ruhusa B ina mambo za kutazamiya ku calendrier zenye zinahusisha mabadiliko ya yenye haiko ya adabu ambayo pendekezo ya kamati ya sheriya inapashwa kupitisha
- Calendrier yenye Inapeana Ruhusa C ina mambo ya kutazamiya ku calendrier yoyote ambayo pendekezo ya kamati inapashwa kurejeya.

Mambo za Kutazamiya ku calendrier zenye ziko na ripoti ya groupe ya kiloko haziwezi kuwekwa kwa Calendrier yenye inapeana ruhusa yoyote. Mambo zenye athari za kimakuta ao mambo zenye zinahusika na Katiba haziwezi kuwekewa mu ma calendrier yenye inapeana ruhusa A ao B, lakini zinaweza kuwekewa kwa calendrier yenye inapeana ruhusa C kwa sababu hakutakuwa na athari za kimakuta ao kikatiba.

## Kanuni ya 33(7) Kutosha Mambo ya Kutazamiya ku Calendrier kutoka kwa Calendrier yenye Inapeana Ruhusa

Bajumbe wowote makumi mbili (20) banaweza kuwa na mambo ya Calendrier yenye inapeana ruhusa kutosha kwa kuwasilisha Formilere ya Ombi ya Kuondolewa Calendrier yenye Inapeana Ruhusa kufikia 3:00 ya mangaribi ya siku mambo ya kutazamiya ku calendrier huonekana kwa mara ya kwanza ndani ya Avocat mu Kristo wa Kila Siku. Formulaire inaweza kuchukuliwa kutoka mu chumba 104 na kurudishiwa mu chumba 104. Bajumbe benye Banachungwa banaweza kutia sinye maombi ya kutosha mambo kwa calendrier yenye inapeana ruhusa bakiwa bameikala tu kama bajumbe wa kupiga kura.

## Kalenda ya Kibali A02

**23**-CC1-¶165-A-G
**Sujets: Kanuni za Kijamaa zenye Zilirekebishwa-164 na 165**
Maombi: 20732-CC-¶165-G
Uanachama: 32; Balikuwapo: 25;
Banaunga Mkono: 25; Banapinga: 0; Kutokupiga Kura: 0;
Tarehe: 4/25
Maombi inabakia kama ilivyoletwa.

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**24**-GA1-¶263.4-A-G
**Sujets: Mabadiliko yenye ilipendekezwa kwa Siku ya Mwanafunzi ya Methodiste Unie**
Maombi: 20250-GA-¶263.4-G
Uanachama: 58; Balikuwapo: 52;
Banaunga Mkono: 49; Banapinga: 1; Kutokupiga Kura: 2;
Tarehe: 4/25
Maombi inabakia kama ilivyoletwa.

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**25**-GA2-¶263.6c-A
**Sujets: Mapendekezo ya Mabadiliko ya Dimanche ya Huduma za Amérindiens**
Maombi: 20251-GA-¶263.6c
Uanachama: 58; Balikuwapo: 52;
Banaunga Mkono: 50; Banapinga: 1; Kutokupiga Kura: 1;
Tarehe: 4/25
Maombi inabakia kama ilivyoletwa.

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**26**-GA3-¶265.4-A-G
**Sujets: Kuhusu Dimanche ya Ufahamu ya Bulemavu**
Maombi: 20252-GA-¶265.4-G
Uanachama: 58; Balikuwapo: 52;
Banaunga Mkono: 50; Banapinga: 0; Kutokupiga Kura: 2;
Tarehe: 4/25
Maombi inabakia kama ilivyoletwa.

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**27**-GA5-¶703-A
**Sujets: Agence ya Utawala**
Maombi: 20256-GA-¶703
Uanachama: 58; Balikuwapo: 52;
Banaunga Mkono: 46; Banapinga: 3; Kutokupiga Kura: 3;
Tarehe: 4/25
Maombi inabakia kama ilivyoletwa.

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**28**-GA6-¶906-A
**Sujets: Marekebisho ya Buanachama wa Table ya Kuunganisha**
Maombi: 20984-GA-¶906
Uanachama: 58; Balikuwapo: 52;
Banaunga Mkono: 48; Banapinga: 1; Kutokupiga Kura: 3;
Tarehe: 4/25
Maombi inabakia kama ilivyoletwa.

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**29**-HS1-¶634.4a6-A
**Sujets: Bufafanuzi ya Ofisi ya Bourse ya Masomo**
Maombi: 20977-HS-¶634.4a6
Uanachama: 68; Balikuwapo: 59;
Banaunga Mkono: 51; Banapinga: 3; Kutokupiga Kura: 5;
Tarehe: 4/25
Approved as submitted

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**30**-HS2-¶634.4-A
**Sujets: Bufafanuzi ya Ofisi ya Bourse ya Masomo**
Maombi: 20978-HS-¶634.4
Uanachama: 68; Balikuwapo: 59;
Banaunga Mkono: 51; Banapinga: 4; Kutokupiga Kura: 4;
Tarehe: 4/25
Approved as submitted

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**31**-HS3-¶1406-A
**Sujets: Kusasisha Majukumu ku Bodi Mukubwa ya Masomo ya Yulu na Huduma**
Maombi: 20979-HS-¶1406
Uanachama: 68; Balikuwapo: 59;
Banaunga Mkono: 56; Banapinga: 0; Kutokupiga Kura: 3;
Tarehe: 4/25
Approved as submitted

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

**32**-HS6-¶1405-A
**Sujets: Kusasisha Malengo ya Bodi Mukubwa ya Masomo ya Yulu na Huduma**
Maombi: 21098-HS-¶1405
Uanachama: 68; Balikuwapo: 55;
Banaunga Mkono: 53; Banapinga: 0; Kutokupiga Kura: 2;
Tarehe: 4/25
Approved as submitted

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

## Ma Article ya Kalenda R02

**33**-CC2-R6001-A-$-G
**Sujets: Université ya Afrique**
Maombi: 20849-CC-R6001-$-G
Uanachama: 32; Balikuwapo: 27;
Banaunga Mkono: 27; Banapinga: 0; Kutokupiga Kura: 0;
Tarehe: 4/25
Maombi inabakia kama ilivyoletwa.

Comite Inapitisha yaliyo hapa yulu

[ ] Imepitishwa [ ] Haijapitishwa Tarehe /